Seventh-Day Adventist® Church
NORTHERN TANZANIA UNION CONFERENCE
SOUTH NYANZA CONFERENCE



# MUONGOZO WA IDARA YA ELIMU

## KWA WACHUNGAJI, WAZEE NA VIONGOZI WA IDARA YA ELIMU KANISANI

Umeandaliwa na:
**Mch. Mwl. Marco. F. Mlingwa.**
MKURUGENZI IDARA YA ELIMU- SOUTH NYANZA CONFERENCE.

## DIBAJI

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa elimu ya kikristo kwa washiriki wa kanisa la waadventista Wasabato na hasa kwa viongozi wanaosimamia idara ya elimu makanisani. Unalenga kutoa ufafanuzi wa idara ya elimu katika ujumla wake. Unaelezea mambo yafutatayo:

1. Misingi ya Elimu ya Kikristo.
2. Falsafa ya Elimu ya Kanisa la Waadventista wasabato na Mafundisho makuu katika falsafa ya Elimu ya kikristo.
3. Malengo ya elimu ya Kiadventista.
4. Mawakala wa Elimu ya Kiadventista.
5. Mfumo wa elimu ya Kiadventista.
6. Uhamasishaji wa umuhimu wa elimu ya kikristo nyumbani, shuleni na vyuoni.
7. Watekelezaji wa uhamasishaji wa elimu ya kikristo
8. Mkakati wa uhamasishaji.
9. Mwongozo wa kuruhusiwa kuendesha shule kwa kutumia jina na mfumo wa kanisa la waadventista wasabato.
10. Shughuli za katibu wa walimu wa kanisa na Kamati ya Elimu kanisani.
11. Taratibu za kuanzisha na kusajili shule.
12. Uinjilisti Kupitia idara ya Elimu.
13. Maelezo ya E.G. White Kuhusu Sifa za Mwalimu.

YALIYOMO

DIBAJI ....... 1
SURA YA 1: MISINGI YA ELIMU YA KIKRISTO ....... 3
SURA YA 2: FALSAFA YA ELIMU YA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO ....... 4
Matawi ya Falsafa ....... 4
Maana ya Falsafa ya Elimu kulingana na Biblia na Roho ya Unabii ....... 4
Falsafa ya Elimu ya Waadventista ....... 4
Mafundisho katika Falsafa ya Elimu ya Kikristo ....... 5
SURA YA 3: MALENGO YA ELIMU YA KIADVENTISTA ....... 9
Vipengele Muhimu Katika Kufikia Malengo Ya Elimu Ya Kiandventista ....... 9
SURA YA NNE: MAWAKALA WA ELIMU YA KIADVENTISTA ....... 13
SURA YA TANO: MFUMO WA ELIMU YA KIADVENTISTA ....... 16
Muundo wa Elimu hapa Tanzania ....... 16
Muundo wa Elimu wa Kanisa la Waadventista Wasabato ....... 17
SURA YA SITA: UHAMASISHAJI WA UMUHIMU WA ELIMU YA KIKRISTO NYUMBANI, SHULENI NA VYUONI ....... 19
i. Elimu ya nyumbani yaonekana kuhamishiwa kanisani/shuleni ....... 19
ii. Elimu ya shuleni kwa mujibu wa umri ....... 19
iii. Elimu ya Vyuoni ....... 19
iv. Jinsi ya kukabiliana na maisha ya shule/vyuo ....... 20
SURA YA 7: WATEKELEZAJI WA UHAMASISHAJI WA ELIMU YA KIKRISTO ....... 21
i. Ngazi ya Kanisa Mahalia ....... 21
ii. Ngazi ya Konferensi ....... 21
SURA YA 8: MKAKATI WA UHAMASISHAJI ....... 22
SURA YA 9: MWONGOZO WA KURUHUSIWA KUENDESHA SHULE KWA KUTUMIA JINA NA MFUMO WA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO ....... 23
Mamlaka ya kanisa na Chimbuko lake ....... 23
SURA YA 10: SHUGHULI ZA KATIBU WA ELIMU WA KANISA MAHALIA/KUNDI ....... 28
Kuchanguliwa kwa Katibu wa Elimu Wa Kanisa ....... 28
Sifa za Katibu wa Elimu Kanisani ....... 28
Majukumu ya Katibu/Karani wa Elimu Kanisani ....... 28
Mapendekezo ya Division ....... 29
SURA YA 11: UINJILISTI KUPITIA ELIMU ....... 30
Faida Za Kuanzisha Shule Katika Kanisa Mahalia ....... 30
SURA YA 12: NINI KIFANYIKE ILI KUBORESHA ELIMU YA KIADVENTISTA KATIKA MAKANISA YASIYO NA SHULE? ....... 34
Nini kifanyike? ....... 34
Mfumo wa Kamati ya Elimu katika kanisa mahalia ....... 36
SURA YA 13: TARATIBU ZA KUANZISHA NA KUSAJILI SHULE ....... 37
Aina za Shule na Maana zake ....... 37
Uendeshaji wa Shule ....... 37
REJEA ....... 41

## SURA YA 1: MISINGI YA ELIMU YA KIKRISTO

Waadventista Wasabato, katika muktadha wa imani yao, wanakiri kwamba:

i. Mungu ni muumbaji na mruzuku wa ulimwengu, vikiwemo viumbe hai na visivyo hai;
ii. Mungu alimuumba mwanadamu mkamilifu katika sura yake akiwa na uwezo wa kufikiri, kuchagua na kufanya mambo;
iii. Mungu ni chanzo cha kila kilicho cha kweli, chema na kizuri na amechagua kujidhirisha kupitia kwa mwanadamu;
iv. Wanadamu kwa uchaguzi wao wenyewe, walimwasi Mungu na kuanguka katika hali ya dhambi ambayo imewatenga na Mungu na imewatenga wao kwa wao na kuathiri dunia nzima na kuitumbukiza katika pambano kuu la ulimwengu kati ya wema na ubaya. Licha ya hali hii, ulimwengu na wanadamu bado wanadhihirisha wema na uzuri wa hali yao ya awali, japo kwa uhafifu,
v. Uungu ulikabiliana na tatizo la dhambi kupitia mpango wa ukombozi. Mpango huu unalenga kumrejesha mwanadamu katika sura ya Mungu na ulimwengu katika hali yake ya awali ya ulinzi, upendo na maelewano.
vi. Mungu anatualika kuchagua mpango wake wa urejeshwaji na kuwa na uhusiano na dunia hii kwa ubunifu na uwajibikaji hadi atakapoingilia kati katika historia na kuumba mbingu mpya na nchi mpya zilizoahidiwa katika Neno lake

## SURA YA 2: FALSAFA YA ELIMU YA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO

Neno Falsafa linatokana na neno Philosophy: Philo - (*Pendo*) - Sophia (*hekima*) **(**kutoka Kigiriki *φιλοσοφία filosofia = pendo la hekima*) ni jaribio la kuelewa na kueleza ulimwengu kwa kutumia akili inayofuata hoja za mantiki. Falsafa huchunguza mambo kama kuweko/kutokuweko, ukweli, ujuzi, uzuri, mema na mabaya, lugha, haki na mengine yoyote.

### Matawi ya Falsafa

i. *Ethics* - ***maadili*** ni elimu ya kutenda mema, chanzo cha maadili ni nini?
ii. *Metaphysics* - metafizikia ni elimu ya ***vyanzo vya kuwepo***, uhai na maarifa
iii. *Epistemology* – epistemolojia ni elimu ya ufahamu inayoeleza chanzo cha ***ukweli***.
iv. *Logic*- mantiki ni elimu ya kutafakari na mfululizo wa dhana

### Maana ya Falsafa ya Elimu kulingana na Biblia na Roho ya Unabii

Falsafa ni ufahamu wa Mungu, na Yesu Kristo, ambaye alimtuma**,** *Ufunuo 14:6, 7; Yohana 17:3; Mithali 9:10.*

### Falsafa ya Elimu ya Waadventista

Falsafa ya Elimu ya kiadventista imejengwa katika dhana ya urejeshwaji wa sura ya Mungu iliyopotea kwa mwanadamu kupitia mwenendo wa nguvu za kimwili, kiakili na nguvu za kiroho. (Ed. 13, 15, 16)

Kanisa huendesha utaratibu wa shule ili kuhakikisha kwamba vijana wake wanapokea elimu yenye uwiano wa kimwili, kiakili, kiroho na kijamii na elimu ya kazi kulingana na viwango na malengo ya kanisa, na Mungu akiwa ndiye chimbuko la thamani kimaadili na ukweli. Shauku ya kanisa ni urejeshwaji wa sura ya Muumba wake ndani ya mwanadamu, ikiwa na matokeo ya maendeleo bora kabisa ya mtu kamili kwa ajili ya yote mawili, maisha ya sasa na maisha baada ya haya.

Kanisa huendesha shule zake lenyewe, kuanzia chekechea hadi chuo kikuu kwa *kusudi la kupitisha kwenda kwa watoto wake malengo yake lenyewe ambayo ni imani, mtazamo, maadili, mazoea na desturi. Shule za kidunia hutafuta kuandaa raia wakereketwa na watiifu kwa sheria za nchi na kufundisha maadili fulani. Shule za kiadventista, zaidi ya hayo, hulenga kukuza wakristo waadventista wasabato watiifu na makini.* Elimu ya kweli ya Mungu, ushirika pamoja na urafiki pamoja naye (Mungu) katika kujifunza na utumishi na kufanana naye katika kukuza tabia ndiyo chimbuko, njia na lengo la elimu ya kanisa la waadventista wa sabato.

## Mafundisho katika Falsafa ya Elimu ya Kikristo

### Fundisho la 1: Umuhimu wa Biblia

Biblia ni Neno la Mungu lililo andikwa, ni ya muhimu sana katika maisha ya Mkristo. Imevuviwa na haina makosa, ina mamlaka kwa maisha yetu yote, ikiwa ni pamoja na maisha ya shule ya Kikristo: *Mithali 3:1, Zaburi 119, Yohana 17:6-19 na Wakolosai 3:16*

*a) Elimu ya Kikristo katika Biblia*

Japokuwa Biblia sio kitabu cha kawaida, hata hivyo huwa inatoa maelezo kuhusu shughuli zote za elimu yetu ya Kikristo katika namna ya msimgi. Zingatia mifano ifuatayo:

i. Biblia inaweza isituambie kama shule inatakiwa kuwa na sheria ya mavazi lakini inatoa mwongozo wa namna gani tunatakiwa tuonekane (uvaaji), maisha yetu yanavyopaswa kuwa kama mtu mmoja mmoja katika jamii tunamoishi. (2Petro 3:3-5)

ii. Biblia inaweza isiwaambie waalimu namna ya kupanga madawati na viti katika madarasa yao lakini inatupatia uelewa kuhusu watoto (walioumbwa kwa mfano wa Mungu, wakaathiriwa na anguko, wanavyowajibika wao binafsi na kwa wenzao katika jamii) hilo linatakiwa kuathiri mpangilio wa darasa la mwalimu.

iii. Biblia inaweza isifafanue namna tunavyotakiwa kufundisha hesabu au sayansi lakini inatuonesha sehemu na mpangilio wa hesabu na sayansi katika ulimwengu wa Mungu. Hesabu na sayansi ni sehemu ya vitu vilivyoumbwa na Mungu na vimejikita katika kiapo cha imani sawa na vitu vinginevyo vyote vinavyoonekana vilivyo katika ulimwengu. Hivyo, ushirikiano wa imani na kujifunza miongoni mwa masomo yote unahitajika.

iv. Biblia inaweza isitoe mifano ya namna gani shule zinatakiwa kukamilisha kadi za taarifa za wanafunzi, lakini bado kupitia katika Biblia tathmini ya kazi yoyote huweza kufanyika. Mfumo wa tathmini katika shule za Kikristo, ambao msingi wake utawekwa katika muundo halisi wa Kibiblia wa vipawa na uwajibikaji (kama ilivyoelezwa, kwa mfano, kupitia ule mfano wa talanta) utampendeza Mungu ambaye tunatafuta kumtumikia maishani.

*b) Utajuaje kwamba Umejifunza*

Mchakato wa kutengeneza mtaala katika shule za Kikristo ni lazima kiini chake kianze na Neno la Mungu (Edlin 1999). Matokeo ya mtazamo wa kibiblia kuhusu maarifa utajumuisha mambo mengi zaidi ya uelewa wa masuala mbalimbali. Katika masharti ya kibiblia, maarifa ya kweli hayapatikani mpaka walimu na wanafunzi wayaishi katika maisha yao. Zingatia mambo ya msingi katika elimu ya kweli:

i. Kulingana na Biblia, ukweli ni jambo ambalo linatakiwa kuthibitishwa na kujilinganisha. Hii ni kwamba, ukweli ni sehemu ya Mungu ya uumbaji

kama iliyo dhihirishwa na ni halisi katika wakati na na inavuka mipaka ya kitamaduni.

ii. Yesu hakuja kutuambia kuhusu ukweli au kutupatia maneno ya kweli. *Yeye ndiye ukweli (Yohana 14:6)*

iii. Kando ya kutumia Biblia katika maombi na mambo ya msingi, Shule ya Kikristo itakita uhusiano wake wote na shughuli zake zote katika maelekezo ya Biblia ili kuhakikisha kwamba kila kitu kinafanyika kwa mujibu wa Biblia pamoja na uelewa wa Kibiblia wa ulimwengu na sehemu yetu na kazi zilizo ndani yake.

iv. Katika kutafuta mwafaka wakati wa kujifunza darasani au nje ya darasa, uelewa halisi wa Biblia katika shule za Kikristo unapaswa kuzingatiwa. Wakati wakutengeneza shabaha/lengo la shule na utekelezwaji wake, uelewa halisi wa Biblia unatakiwa uruhusu kutofautiana/utofauti katika masuala mengine yasiyo ya kiroho.

v. Walimu na wanafunzi wanalazimika kutathmini mitazamo yao kuhusu Elimu na maisha kwa kuzingatia Neno la Mungu, ambalo lengo lake ni kumtukuza Mungu na kuishi kwa ajili ya Yeye katika yote wanayo yafanya

Fundisho la 2: Mtazamo wa kibiblia.

i. Kamwe elimu haiko upande wo wote. Elimu ya Kikristo ni lazima ihakikishe kwamba wanafunzi wanajifunza kuhusu ulimwengu na mahali pao na kazi zilizomo ndani yake katika mtazamo wa jumla wa kibiblia.

ii. Katika Matendo ya Mitume 17, Paulo anatoa hotuba yake mashuhuri sana kwa Waathene kwenye mlima Mars. Katika hotuba hiyo alitangaza kwamba hakuna namna maisha yanaweza kuishi kwa kukosa dini, yaani mtu hawezi kuishi bila dini.

iii. Jambo ambalo waalimu wa Kikristo wanapaswa kujikita kabisa kwalo ni tamko la ushirikiano uliopo baina ya imani na kujifunza (Integration of faith with learning).

Fundisho la 3: Umuhimu wa Wazazi.

i. Mungu amewapatia wazazi jukumu la msingi la kuwalea watoto wao. Shule za Kikristo hushirikiana na wazazi ili kuwasaidia katika kutimiza majukumu yao.

ii. Kuna majukumu ambayo ni ya wazazi toka kwa Mungu: Kuwalea watoto wao katika nidhamu na maelekezo ya Bwana. Jukumu hili ni kwa kila mzazi na mlezi (Mwalimu) ambaye anapaswa kutoa malezi bora kimwili, kiroho, na kielimu kwa watoto wa Mungu.

iii. Shule za Kikristo ni lazima ziwezeshe ushiriki wa wazazi katika maisha ya shule. Shule za Kikristo hazitakiwi kuwaogopa wazazi bali ziwatie moyo kuhusika katika masuala mbalimbali ya maendeleo ya shule kiroho na kielimu kwa uwiano sahihi.

iv. Shule za kikristo zinatakiwa kuwa na tahadhari ya lugha, miundo, na tamaduni za shule ambazo zitawafanya wazazi wasitimize wajibu wao kwa ukamilifu.

### Fundisho la 4: Umuhimu wa Waalimu

Shule za Kikristo hazitafaulu endapo hazitakuwa na walimu ambao wanaelewa vyema, wanafundisha na kuishi kutokana na mtazamo mwema wa kibiblia. Shule zinatakiwa kuwapatia walimu wao maendeleo ya kitaaluma yenye kujitosheleza na ya uthibitisho wa kibiblia. *(Tazama Luka 6; 40; 1Thesalonike 2:8)*

*Wajibu wa Waalimu*

Waefeso 4 inatukumbusha kwamba ofisi ya walimu inapaswa kutawaliwa kibiblia. Walimu wanapaswa kuwa na vipaji au uwezo unaoendana na wito wao. Shule zinatakiwa ziundwe katika namna ambayo inawaruhusu kuweka katika vitendo hivyo vipaji vyao katika namna ambayo inamheshimu Mungu.Tamathali za semi zilizotumiwa na Van Brummelen (1998)-mwana sanaa, mwezeshaji, msimulia hadithi, wakili, kuhani, na kiongozi –inatoa picha ya kazi mbalimbali za mwalimu Mkristo. Walimu wa Kikrsto ni lazima wafanye kazi katika jamii.

### Fundisho la 5: Malezi katika shule za Kikristo

i. Watoto ni wabeba sura ya Mungu na viumbe waliobarikiwa, lakini wameathiriwa na anguko na wanahitaji ukombozi katika Kristo. Shule zinatakiwa ziwasaidie waone amani ya Mungu na kusudi la Mungu kwa maisha yao na uliwemngu wao kama mawakili wanaowajibika kwa Mungu.

ii. Wanafunzi kama wabeba sura wa Mungu, pia wanalo hitaji la kufanya chaguzi za kimaadili na kuwajibika kwa chaguzi hizo. Kwa hiyo, uwalimu katika shule za Kikristo unakwenda mbali zaidi ya kufundisha moja kwa moja, unajumuisha kujifunza kwa namna ambayo walimu na wanafunzi kwa pamoja wanajifunza kuhusu ulimwengu na mahali pao na kazi zilizomo ndani yake. Nidhamu haitakiwi kutenganishwa na malezi bali inataiwa ijikite katika ukweli, kukiri na matengenezo kwa kutumia mfano wa nidhamu (discplining model).

### Fundisho la 6: Uanafunzi na Mwitikio na Shule za Kikristo

i. Elimu ya Kikristo haihamasishi tu ukuaji binafsi. Inawaandaa vijana kutangaza ujumbe wa Mungu ulio wa matumaini na amani katika Kristo. Katika kila shughuli na kazi kwa kizazi kilicho potea na chenye kuhuzunisha, shule zenye msukumo wa utume zinahitajika.

ii. Shule za Kikristo hazitakiwi kuwepo ili zitengeneze kizazi kingine cha wakalia mabenchi. Zinatakiwa ziwaandae vijana pindi wanapomjua Mfalme wa wafalme wawe mabalozi wake katika ulimwengu, wakitafuta kuleta amani katika maisha yote. Huu ndio uanafunzi wenye mwitikio (1Petro 2:9-12).

iii. Maisha ya shule za Kikristo yanatakiwa yawaandae vijana Wakristo katika kila kazi kukosoa jamii zinazoabudu sanamu ambazo wanaishi ndani yake na kuzipelekea ujumbe wa Mungu ulio wa matumaini, amani, na mapatano.

iv. Kama shule za Kikristo zinafanya kazi yao kama inavyoktakiwa, walimu na wanafunzi wao ni lazima wawe chumvi na nguzo ya nuru ya matumaini katika jinamizi hili la kizazi kipya. Kwa kumwakilisha Mungu na njia zake kama ambavyo wamefundisha na kujifunza shuleni, wanayo fursa ya kusimama imara wao wenyewe na kuupelekea amani ya Mungu ulimwengu huu uliokata tamaa na wenye uhitaji.



**Note 1: Mchakato wa kutengeneza mtaala katika shule za Kikristo ni lazima kiini chake kianze na Neno la Mungu.**

## SURA YA 3: MALENGO YA ELIMU YA KIADVENTISTA

Shule zinazoendeshwa na kanisa zitajitahidi kutoa kwa wanafunzi wake wote elimu ndani ya mfumo wa Sayansi ya wokovu. Misingi na matawi ya kawaida ya maarifa sharti yatafitiwe ili kuendeleza ustadi katika matumizi yake. Kwa dhahiri, shule za kanisa zitajitahidi kuendeleza kwa kila mwanafunzi ainue kiwango cha kanuni za afya na kiasi chini ya agizo la utaratibu wa msingi wa kujifunza na katika ufundishaji wa stahili ya uanakaya, mafunzo ya ufundi, elimu ya jamii na utumiaji unaofaa wa fursa ya mapumziko na upevu wa kimaadili. Shule za kiadventista zitalenga kufikia shabaha za kujitoa, kiroho, kujitambua, urekebishaji kijamii, kuwajibika katika jamii, utume ulimwenguni na utumishi na kujitosheleza kiuchumi kwa kiwango cha juu kupitia mafundisho yaliyojengwa katika Kristo.
Thamani ya Elimu ya Kiadventista huweza kuonekana kupitia ujumuishaji wa mafunzo yaliyojengwa katika nyanja zote za maisha. Elimu hii hutolewa ili kumwandaa mtoto kiroho, kiakili, kimwili na kihisia. Huku ikizingatia malengo yafuatayo:

i. **Huduma**- Elimu ya kiadventista humwandaa mwanafunzi kwa ajili ya furaha ya huduma katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao (Ed. 13)
ii. **Ukombozi** –Kazi ya Elimu na kazi ya ukombozi ni moja (Ed.30)
iii. **Urejeshwaji** – Elimu ya kweli itolewayo katika kanisa la Waadventista wa Sabato imejengwa katika kurejeshaji wa taswira ya Mungu iliyopotea kwa mwanadamu kutokana na anguko dhambini (Ed. 15). Juu kuliko mawazo ya juu mwanadamu anayoweza kufikia ndiyo ubora Mungu anaoutaka kwa ajili ya watoto wake (Ed. 18).
iv. **Elimu iliyokamilika-** ukuaji kwa ulinganifu kimwili, kiakili na kiroho (Ed. 18,19
v. **Kukuza tabia njema** inayokubalika ndani na nje ya kanisa (Ed. 18)
vi. **Kufikia Hitaji kuu la Ulimwengu –** “*hitaji kuu la ulimwengu ni watu-watu ambao hawatanunuliwa wala kuuzwa, watu ambao ndani ya roho zao ni wakweli na waaminifu, watu ambao hawaogopi kuita dhambi kwa jina lake, watu ambao dhamiri zao ni kweli kwa wajibu kama sindano ya dira, watu watakaosimamia haki hata ingawa mbingu zishuke” (Ed. 57)*

### Vipengele Muhimu Katika Kufikia Malengo Ya Elimu Ya Kiandventista

Pamoja na mamlaka tatu za elimu ya Kiadventista kama zilivyokwisha ainishwa hapo juu, yaani elimu nyumbani, katika kanisa mahalia na elimu katika shule au vyuo vya kiadventisa, vipengele vifuatavyo pia ni muhimu kuzingatiwa katika kufikisha malengo ya Elimu ya kiadventista ikiwa vitazingatiwa katika taasisi za elimu. (ECD, WP FE 10)

i. Mwalimu

- Ni mtendaji pamoja na Kristo- Ed.30
- Mwakilishi wa Mungu – Edu 33, 287 na CT 267
- Ameitwa kama mmissionari – Ed. 47- 48, 219 -221
- Ni wakala wa uvuvio wa Mungu. Ed. 29.
- Mhamasishaji wa Elimu ya Kiadventista (GC-WP, FE 60).
- Anapaswa kuwa na taaluma sahihi kulingana na elimu aitoayo kwa walengwa, mshiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato na mwenye msimamo mzuri kiimani ( GC- WP, FE: 65.
- Mwalimu katika shule za Kiadventista ni mzazi na mlezi pia kwani anakaa na mtoto kwa muda mrefu kuliko wazazi wa kibaiolojia.
- Ni Nabii – anamlea mtoto kitabia na kiakili na kumwaanda kwa siku za usoni. Anauwezo wa kumweleza mtoto kile kinachoweza kutokea maishani mwake ikiwa mtoto ataamua kufuata njia Fulani iliyo sahihi au mbaya kwa kuzingatia maelekezo ya neno la Mungu, wazazi, wahubiri na sheria zilizowekwa katika jamii.
- Ni Kiongozi wa kiroho (Mchungaji na kuhani) – anayepaswa kusimamia, kuongoza, kutembelea, kushauri, kuwafahamu watoto, kuwapenda, kuwalinda, kuwaombea, kujitoa kikamilifu kwa ajili ya watoto, kuwajali na kuwafundisha watoto waliowekwa chini ya uangalizi wake. Yer. 13: 20. Kumb 6: 6-9.
- Akumbukaye kuwa Yesu ndiye mwalimu mkuu. Ed. 73- 83.

ii. Mwanafunzi

- Ameumbwa kwa mfano wa Mungu- anapaswa kuthaminiwa, kuchukuliana naye na kukubalika kwa jinsi alivyo. Mw. 1:26, 27 na 31, Ed. 79.
- Ana uwezo wa kiakili. CT 73
- Anaweza kujaribiwa na kuanguka dhambini. Ed. 292, 293, 294, 289.
- Ni hekalu la Mungu. Ed. 201.
- Ikumbukwe kuwa hatima ya mwanafunzi ni kipimo kikubwa cha kuonyesha ufanisi wa taasisi na ubora wake.

iii. Shule

- Kila shule yapaswa kuwa “mji wa kimbilio” Ed. 33, 293; CT 269
- Uzio au kizuizi dhidi ya uasi unaoenea duniani Ed.46.
- Taasisi ya kuhekimisha, kituo cha mafunzo katika Nyanja zote na kiwanda cha kuzalisha watu bora kwa dunia ya sasa na kwa umilele.Ed.218.
- Tawi la shule ya mbinguni. Ed 30

iv. Chanzo cha Maarifa

- Elimu itolewayo katika shule za kanisa imejengwa katika msingi wa imani kwa Mungu na na mtazamo wa kiroho kwa kuthamini uumbaji na mpangililio halisi wa viumbe vya asili siyo ufahamu wa kisayansi tu.

v. Mtaala

- Mtaala katika shule za kiadventista umeandaliwa kuhamasisha ubora wa kitaaluma kupitia masomo yanayomwandaa msomaji kuwa raia mwema kwa ulimwengu wa sasa na na kwa umilele. Masomo kama Kuthamini urithi wa kanisa la Kristo, Kujali haki ya jamii na uwakili wa mazingira yanapotolewa katika uwiano mzuri humwandaa mwanafunzi kuwa raia mwema katika jamii aishiyo na hata katika mbingu mpya. Mtaala wenye uwiano sahihi utazingatia hitaji la maendeleo muhimu kiroho, kiakili, kimwili, kijamii, kihisia, pamoja na elimu ya kazi. Masomo yote yatalenga katika mtazamo wa kibiblia na ujumbe ulio katika pambano kuu.

vi. Kufundisha na Kujifunza.

- Program za kufundisha na kujifunza madarasani husisitiza katika mifumo yote ya elimu ya kweli na zimelenga katika kuhusianisha imani na kujifunza *(integration of faith with learning)*. Mbinu za kufundishia ni zile zinazomhusisha mwanafunzi Zaidi na zenye kugusa mahitaji yake kulingana na uwezo wake kiakili. Baada ya kutumia mbinu hizi matarajio ni kumfanya mwanafunzi aweze kuyaweka masomo katika matumizi maishani, kuwa na nidhamu na utii kwa sheria za tamaduni husika.

vii. Nidhamu.

- Nidhamu katika shule za kanisa imejengwa juu ya hitaji la kurejesha taswira ya Mungu kwa kila mwanafunzi na kutambua mapenzi ya Mungu na utendaji wa roho mtakatifu.

viii. Maisha ya Shule

- Msisitizo mkubwa umewekwa katika ibada, masomo, kufanya kazi, michezo, na mahusiano ambavyo vinahusianishwa katika mazingira ya kujifunza. Maisha ya wanajamiii katika taasisi za shule yamegubikwa na mambo ya kiroho, ushirikiano na kuheshimiana bila kujali tofauti za tofauti za watu na tamaduni zao.



**Note 2: Thamani ya Elimu ya Kiadventista huweza kuonekana kupitia ujumuishaji wa mafunzo yaliyojengwa katika nyanja zote za maisha. Elimu hii hutolewa ili kumwandaa mtoto kiroho, kiakili, kimwili na kihisia.**

## SURA YA NNE: MAWAKALA WA ELIMU YA KIADVENTISTA

Elimu ya kiadventista inafanyakazi kupitia mawakala wakuu wanne ambao ni

**i. Elimu Nyumbani**

Elimu ya kiadventista huanzia katika nyumba zetu ambapo hutolewa na wazazi kwa watoto wadogo, miaka 0 – 8. *"Ni katika nyumba zetu ambapo elimu ya mtoto inapaswa kuanzia. Hapa ni shule yake ya kwanza. Hapa akiwa na wazazi wake kama waalimu anajifunza masomo ambayo yatamuongoza katika maisha yake yote - masomo ya staha, utii, kicho, kujidhibiti. Mvuto wa elimu ya nyumbani ni nguvu iliyoamuliwa kwa wema au kwa ubaya. Mvuto huo kwa namna mbalimbali ni wa kimya kimya na wa taratibu, lakini kama mvuto huo ukiwa katika upande sahihi huwa ni nguvu kubwa kwa ajili ya ukweli na haki. Kama mtoto hatafundishwa vizuri nyumbani, shetani atamfundisha mtoto huyo kupitia mawakala wake atakaowachagua. Shule ya nyumbani ni muhimu kiasi gani sasa*?" *(*Ellen G. White, Child guidance, uk.17). Je, tunaanda mazingira mazuri nyumbani kwa ajili ya maendeleo ya kitabia na kimaadili kwa watoto wetu? Je, nyumba zetu ni mbingu ndogo hapa duniani? Je, tunasoma Biblia pamoja na watoto wetu? Je, tunawasomea Biblia watoto wetu? Je tunaomba na watoto wetu? Je, tunawaombea watoto wetu? Ili nyumba zetu ziwe shule nzuri kwa watoto wetu ni lazima tuwekeze mali na muda wetu katika shule hiyo. *Ikumbukwe kuwa shule ya nyumbani haina likizo wala haina kipindi wazi. Wakati wote ni wa kujifunza na kufundisha (*Kumb. 6: 6-7*)*. Mzazi au mlezi anapaswa kutambua kuwa uko darasani wakati wote; ulalapo uko darasani, kuna mtoto anajifunza, unywapo, utembeapo, unenapo, uvaapo, ufurahipo, na ufanyapo kazi nyumbani kwako uko darasani kuna mtu anajifunza kupitia kwako!

**ii. Elimu Katika Kanisa Mahalia**

Elimu ya kiadventista huota mizizi katika kanisa mahalia. "*Mungu amelichagua kanisa kuwa mlinzi ili liwatunze kwa uangalifu mkubwa vijana na watoto na kushika doria ili kuwaona maadui wanapokaribia na kutoa tahadhari dhidi ya hatari. Lakini kanisa halitambui hali hii! Kanisa limesinzia lindoni*" (*Counsels to Parents, Teachers and Students, uk .165*). Je, tunategemeza kikamilifu elimu ya kiadventista katika kanisa letu mahalia? Tunafanya nini kusaidia kupatikana kwa fursa ili watoto wengi kwa kadri iwezekanavyo wapate elimu ya kiadventista? Hatima ya umilele kwa watoto wetu ipo hatarini. Ikiwa Idara mabalimbali za kanisa hazitafanya majukumu yake vilivyo kwa mfano viongozi wa kanisa kupuuzia baadhi ya idara wakati wa kuchagua viongozi wake (mfano idara ya watoto kutopewa kipaumbele na badala yake viongozi wa watoto kuchaguliwa baada ya nafasi zingine kuwa zilishajazwa, kwa hakika kitendo hiki kinahafifisha maandalizi ya wachungaji, wazee na mashemasi wa kanisa la kesho). Tafakari kidogo kwa kujiuliza maswali haya: Je, kanisa lako lina waalimu wa watoto? Je, walimu wa watoto wanasoma lessoni zao kila siku kabla ya kufundisha? Je kanisa lako lina idara za vijana zilizo hai (wavumbuzi, watafuta njia, mabalozi, na AY)? Idara hizi zinafanya kazi zake za uinjiliti ndani na nje ya kanisa? Ikumbukwe kuwa Maisha si tu kupata alama za juu darasani na vyeti au shahada, kumbuka kuna jehanamu pia ambayo ni lazima watoto wetu waikimbie na pia kuna mbingu ya kukimbilia.

**iii. Taasisi za Elimu za Kiadventista (Shule na Vyuo)**
Elimu ya kiadventista shuleni hutolewa na waalimu kwa kufuatiliwa na wazazi kwa watoto wa umri wa miaka 6/7 – 15/18. Elimu ya vyuoni hutolewa na wakufunzi kwa kusimamiwa na KANISA kwa vijana wa umri wa miaka 19 – 24/25. Ellen G. White anaonya kuwa "*Katika wakati huu wa hatari kubwa kwa vijana, majaribu yanawazunguka kila upande; na wakati ambapo ni rahisi kwa vijana kuchukuliwa na mawimbi ya majaribu, nguvu kubwa sana inahitajika ili kukabiliana na mawimbi hayo. Kila shule ya kiadventista inapaswa kuwa mji wa kimbilio kwa vijana walio majaribuni, mahali ambapo matatizo yao yanapaswa kushughulikiwa kwa subira na busara (*Ellen G. White, Education, uk. 293). *Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo (*Wakolosai 2:8*)*. Elimu-dunia inaweka maandiko matakatifu pembeni. Elimu endelevu yeyote pasipo Biblia ni ya mtazamo wa kibinadamu.

Tunafanya nini kama mshiriki mmoja mmoja, familia na kanisa mahalia kuhakikisha kwamba shule za kanisa zina rasilimali za kutosha ili ziwe "mji wa kimbilio", vituo vya uinjilisti na ubora wa kitaaluma? Je, inawezekana shule zetu za kanisa hazifanyi vizuri kwa sababu ya kutotegemezwa kutoka kwa washiriki na kanisa mahalia? Lengo letu ni kwamba, kwa neema ya Mungu, shule zetu ziweze kuwasaidia vijana kufaulu vizuri katika mitihani ya taifa na wakati huohuo kuwaanda kwa umilele. Tunatoa changamoto kwa washiriki na kanisa mahalia kuzitegemeza shule za kanisa kwa kuongeza michango yao ya hali na mali kwa shule hizi ili ziwaandae vizuri vijana wetu kwa maisha ya duniani na kwa umilele.
Shule za kanisa zinajengwa kwa kusudi la kuweka uzio katika maisha ya wanafunzi dhidi ya uharifu uliosambaa duniani. Pia, kuwajenga vijana kiakili na kiroho huku zikiwaandaa vijana hao kuwa wakereketwa kwa mafanikio na ujenzi wa taifa lao na utumishi kwa kanisa la Mungu. (Ed. 46)

**iv. Kanisa la Ulimwengu**
Kanisa la ulimwengu limepewa wajibu wa kuangalia na kusimamia utendaji, ubora na ufanisi katika kujifunza kupitia mamlaka zote zilizotajwa hapo juu. Kwa kuzingatia shule zikiwa kama mamlaka za kielimu, jukumu la shule linaweza kufanyika kwa kuongeza shule na kuhamaisisha ujenzi wa shule Zaidi. Hali itakayosaidia kuwahakikisha kuwa kila mtoto wa Kiadventista anapata fursa ya kusoma katika shule au taasisi ya Kiadventista. Kwa kutambua kuwa asilimia

kubwa ya watoto wa kiadventista hawasomi katika shule au vyuo vya Kiadventista, kanisa la Ulimwengu lina jukumu la kutafuta njia za kufikia malengo ya Elimu ya Kiadventista kupitia njia mbadala kama: mafunzo ya kiroho baada ya watoto kutoka shuleni, kuandaa vituo vya mafunzo ya yaliyofadhiliwa na kanisa katika taasisi zisizo za kanisa na hata vipindi vya dini mashuleni katika shule au vyuo vya serikali.



**Note 3: Elimu ya kiadventista shuleni hutolewa na waalimu kwa kufuatiliwa na wazazi kwa watoto wa umri wa miaka 6 – 18. Elimu ya vyuoni hutolewa na wakufunzi kwa kusimamiwa na KANISA kwa vijana wa umri wa miaka 19 – 25**

## SURA YA TANO: MFUMO WA ELIMU YA KIADVENTISTA

Kabla kuuelewa mfumo wa Elimu ya kiadventista angalia yafuatayo juu ya mfumo wa elimu na ufafanuzi wake:

a. Mfumo wa utendaji wa taasisi yo yote kwa sehemu kubwa huathiriwa na falsafa ya taasisi hiyo.
b. Mfumo wa Elimu wa kanisa la Waadventista Wasabato umejengwa juu ya falsafa ambayo chimbuko lake ni imani itokanayo na mafundisho ya kibiblia, pamoja na ufafanuzi utokanao na maandiko ya Ellen G. White kuhusiana na mfumo wa Elimu ya Kikristo.
c. Mfumo wa Elimu wa Wizara ya Elimu Tanzania, haukujengwa juu ya imani itokanayo na mafundisho ya kidini; bali umetokana na utafiti wa kisayansi unaozingatia maoni au mapenzi ya watu, jamii, na maarifa yaliyopo kuhusiana na utayari wa akili ya mwanadamu kupokea elimu (maarifa). Sera za elimu chini ya mfumo huu huendana na mamlaka zote zihusikanazo na utafiti, uchunguzi wa kisayansi, na maoni ya watu jamii (siasa); yakizingatia maoni ya kimila, au desturi za kiutamaduni, kwa kutegemea wakati na mahali, au viwango vya elimu itolewayo, iwe ni ya awali, msingi, sekondari, chuo au ya ufundi, na kadhalika.
d. Elimu ya kikristo, mfumo wake na sera zake hutegemea sana kanuni za kibiblia za uelimishaji au uhamishaji wa maadili toka kizazi kimoja kwenda kingine, au maoni ya kimazingira, utamaduni au mila za watu na jamii. Kwa lugha nyingine, kanuni hizi zaweza zisilazimike kuridhia utafiti uliofanywa na wasomi kiasayansi.
e. Changamoto kubwa inayolikabili kanisa na utendaji wake ni kujifunza jinsi ya kuoanisha mfumo wake wa utendaji na mfumo unaotumiwa na Serikali ambayo ndiyo yenye usimamizi na yenye kuratibu shughuli zote za kielimu nchini. Hatua ya kwanza ya kukabiliana na changamoto hii ni kila upande uelewe misingi ya mfumo wa upande mwingine kisha mkakati ufanywe wa kufungamanisha mifumo miwili inayotokana na sera mbili tofauti, ndani ya progamu moja ya kielimu.

Hatua hii ni muhimu kufanyika kwa sababu kanisa liko ndani ya jamii, likielimisha jamii, kwa kuzingatia mahitaji ya watu jamii, na lenyewe likiwa ni sehemu ya jamii. Wakati huo huo, kanisa lina miiko ya utendaji unaotokana au unaoelekezwa na mafundisho ya imani inayoweza kutofautiana na mapenzi ya watu na jamii, na hivyo kulazimika kutetea imani yake pale inapoonekana muhimu kufanya hivyo.
Katika kipengele hiki, mifumo ya aina mbili italinganishwa ambayo ni mfumo au muundo wa elimu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano waTanzania na muundo wa elimu ya Kikristo katika kanisa la waadventista wasabato.

### Muundo wa Elimu hapa Tanzania

i. Muundo wa elimu ulio rasmi (formal education and training system) kwa Tanzania bara una ngazi zifuatazo***:***
    a) Miaka 2 ya elimu ya Awali – (Umri wa 5 – 6)
    b) Miaka 7 ya Elimu ya Msingi – (Umri 7 – 13).

c) Miaka 4 ya Elimu ya Sekondari – (O – level) (Umri 14 – 17)
d) Miaka 2 ya Elimu ya Sekondari – (A – level) Umri 18 – 19).
e) Miaka isiyopungua 3 ya Elimu ya Chuo Kikuu (Umri 20 – 23 +++).
f) Kwa kifupi muundo huitwa 2 – 7- 4- 2- 3+.
g) Elimu ya mafunzo ya ufundi (Vocational education), ni program maalum baada ya elimu ya nadharia na vitendo

Muundo huu unategemewa utekelezwe na ngazi zifuatazo:

a) Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi.
b) Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).
c) Taasisi ya Elimu.
d) Taasisi zisizo za kiserikali, mfano mashirika ya dini na kadhalika.
e) Watu binafsi wanaoendesha huduma za elimu wanaoratibiwa na Serikali Kuu.

ii. Muundo wa elimu ulio rasmi (formal education and training system) kwa Tanzania Zanzibar una ngazi zifuatazo***:***

a) Miaka 7 ya Elimu ya Msingi- Umri wa miaka 7- 13.
b) Miaka 3 ya Elimu ya Sekondari ya Awali – Umri wa miaka 14-16.
c) Miaka 2 ya Elimu ya Sekondari ya Pili – Umri wa miaka 17-18.
d) Miaka 2 ya Elimu ya Sekondari ya juu- Umri wa miaka 19- 20.
e) Mfumo wa Elimu baada ya Sekondari ya juu unafanana na wa Tanzania bara.
f) Kwa kifupi Muundo huu huitwa 7-3-2-2-3+

Serikali imeweka sera za kuelekeza mfumo wa Elimu kuanzia Elimu ya awali hadi Elimu ya Chuo Kikuu; sera ambazo taasisi zote, zisizo za kiserikali pia zinapaswa kuzingatia. Rejea ***Sera ya Elimu na Mafunzo*** kwa ufafanuzi zaidi. Waweza kupitia kwa makini ili kupata mwelekeo katika uhusiano wa mfumo wa Elimu wa kikanisa na wa kiserikali, katika harakati za kuboresha elimu itolewayo chini ya mfumo wa kikanisa.

### Muundo wa Elimu wa Kanisa la Waadventista Wasabato

Kwa mujibu wa falsafa ya kanisa la Waadventista Wasabato ngazi inayosimamia utekelezaji wa mfumo wa Elimu ikiwemo mabadiliko ya muundo wa mfumo ni ***Kanisa la Ulimwengu***. Ngazi hii kwa kutumia bodi za Elimu za ngazi mbali mbali, huchunguza uwezekano wa:

i. Kuanzishwa kwa muundo wa shule za elimu ya awali;
ii. Kuanzishwa kwa muundo wa shule za elimu ya watu wazima iliyolenga malezi na maadili ya kikristo kwa watu wazima waliokosa elimu hiyo ndani ya utaratibu wa kawaida wa taasisi za elimu (After-school church – based instruction);
iii. Kuanzishwa kwa vituo vya kutolea elimu katika maeneo yasiyomilikiwa na Kanisa la Waadventista Wasabato (church-sponsored centres on non-Adventist campuses;

Ni kwa kuzingatia muktadha huu, Kanisa la Waadventista Wasabato linakubali kuendesha shule za aina 4 au 5 kama ifuatavyo:

i. **Shule za Kanisa (Church Schools)**
    - Mmiliki na mwendeshaji ni kanisa katika ngazi yo yote iliyohiari kujenga na kuendesha shule kwa gharama za ngazi hiyo, kwa kuzingatia sera zilizowekwa na kanisa. Ni shule zilizolenga kuwanufaisha watoto wa washiriki wa Kanisa, kwa asilimia 75.

ii. **Shule za Kijamii (Community - Church Schools)**
    - Ujenzi na umiliki waweza kuwa ni shirikishi baina ya Kanisa na jamii inayohusika.
    - Kanisa laweza kupewa uendeshaji kwa kutumia sera mseto, za kikanisa na za kijamii, Kanisa likiwa na sauti ya utawala.
    - Ni shule za Uinjilisti zaidi kuliko za kimaadili.

iii. **Shule Zinazofadhiliwa na Serikali (Grant Aided Schools)**
    - Serikali imezijenga na ndiyo inayosimamia menejimenti yote.
    - Kanisa limepewa kuziendesha kwa kutumia watumishi wake n.k.
    - Kanisa halina utawala wa kimaelekezo juu ya aina ya wanafunzi wanaopaswa kusajiliwa au kufukuzwa (Kimaadili).
    - Kanisa linaziendesha kwa kutumia mvuto wake zaidi kuliko sheria zitokanazo na sera za mfumo wake.

iv. **Shule Maalumu kwa Makundi Maalumu (Home School or Directed Home Study)**
    - Wanafunzi ni maalumu wanaolazimika kupata elimu tofauti na ya nchi wanayoishi – hasa wamishenari.
    - Vituo vya shule hizi vinawekwa na Unioni au Konferensi kwa kuzingatia mahitaji na hivyo muundo hutegemea mazingira

v. **Shule Zilizojengwa kama Vituo vya Uinjilisti**
    - Shule imejengwa na Kanisa na inaendeshwa na kanisa.
    - Shule iko katika eneo ambalo Kanisa halina washiriki, hivyo imekusudiwa iwe ni njia mojawapo ya kufanya utume wa kanisa na maadili yanayohimizwa na Kanisa yaenezwe kwa jamii.
    - Kama itaonekana kuwa maadili haya hayaenezwi licha ya kuwepo kwa shule hiyo, basi ni bora ikafungwa.

## SURA YA SITA: UHAMASISHAJI WA UMUHIMU WA ELIMU YA KIKRISTO NYUMBANI, SHULENI NA VYUONI

### i. Elimu ya nyumbani yaonekana kuhamishiwa kanisani/shuleni

- Day care centres zinasaidia wazazi waliokosa muda kukaa na watoto wao.
- Nursery schools (Chekechea) zinasaidia kuwaandaa watoto kuingia darasa la kwanza, lakini mzazi akiwajibika zaidi.
- Mzazi aliye na uwezo aajiri mwalimu wa mtoto ili afundishiwe nyumbani kwao, kumkinga na mazingira ya uambukizi wa maadili kwa kuwa ni mdogo na anaiga kwa upesi. Elimu ya nyumbani ni jukumu ambalo mzazi hawezi kukwepa faida zake na hasara za kukosekana kwake.

### ii. Elimu ya shuleni kwa mujibu wa umri

- Mtoto wa chini ya miaka minane asipelekwe shule za Bweni; akae na wazazi hadi miaka minane ipite;
- Baada ya miaka minane, mtoto akilazimika kuwa Bweni mzazi amtembelee kila wakati kuelewa anavyojifunza mambo mbali mbali.
- Wazazi wawe marafiki wa waalimu wa watoto wa umri wa miaka 10 – 12.
- Waalimu washirikiane na wazazi kurekebisha tabia za watoto kati ya miaka 13 –16.
- Waalimu na wazazi watumie urafiki mzuri miongoni mwa vijana ili kuwarekebisha vijana kimaadili kati ya miaka 17 – 20.
- Vijana wanaozidi miaka 18 waelimishwe kuchukua majukumu na matokeo ya maamuzi yote wanayofanya kwa kauli au kwa vitendo baada ya kufikia umri huo, bila kuwalaumu wazazi au waalimu.
- Nidhamu ya shule hutetewa kwa kutumia adhabu mbalimbali, zikiwemo za kuachishwa shule.

### iii. Elimu ya Vyuoni

- Wahusika ni mchanganlyiko wa marika: Vijana na watu wazima (wazazi kwa wasio wazazi).
- Falsafa ya chuo hutoa mwelekeo wa elimu iliyokusudiwa na maadili yanayotetewa.
- Kanuni na miongozo ya shule (Handbooks/Bulletins/School manual) hutoa maelekezo ya mambo muhimu yakuzingatiwa na kila mwanachuo katika mazingira aliyomo.
- Nidhamu ya shule inatetewa kwa viwango vya chini vya adhabu za kuachishwa chuo, isipokuwa pale inapoonekana kuwa ni kitaaluma zaidi. Kuna jaribu la kuvumilia uovu uliofanywa na wanafunzi/waalimu kwa viwango visivyofanana na elimu ya shule.

### iv. Jinsi ya kukabiliana na maisha ya shule/vyuo

Kama matokeo ya kipengele cha (3) na (4) hapo juu wanafunzi na wanachuo waweza kusaidiwa kukabiliana na changamoto zilizo mashuleni kwa kufanya yafuatayo:

- Kuanzisha na kujiunga katika umoja wa vyama vya kidini. Mfano ASSA, TUCASA, AY, Pathfinder, Adventurer na kadhalika na kuendesha shughuli zihusianazo na vyama hivyo;
- Kuhudhuria mikutano ya vyama hivyo kwa kulipiwa gharama na wazazi/walezi wao;
- Kuwa na walezi wa kiroho mashuleni (Patron na Matron) wanaosimamia, malezi ya kiroho kwa shule zinazoendeshwa kikanisa, na pawepo na wakuu wa kundi au walezi wa kiroho kutoka kanisa lililo jirani na shule ili kutoa huduma kwa vijana waadventista walio katika vyuo au shule zisizo za kanisa;
- Kila Kanisa kupangiwa shule zilizo katika eneo lake na kusimamia uendeshaji wa kipindi cha dini kwa kumweka mwalimu aliyechaguliwa na Kanisa, anayekutana na wanafunzi kila wiki. Mwongozo wa kufundishia unapatikana kwa mkurugenzi wa Elimu wa konforensi. Kila kanisa lihakikishe linapata mwongozo huu;
- Kwa kutegemea na umri wao, wazazi kuingilia kati kwa kupendekeza mambo yanayofaa kufanywa kwa ajili ya watoto, kwa kutumia mikutano ya wazazi inayoitishwa na wazazi au na uongozi wa shule.



**Note 4: Wanafunzi na wanachuo waweza kusaidiwa kukabiliana na changamoto zilizo mashuleni kwa kuanzisha na kujiunga katika umoja wa vyama vya kidini. Mfano ASSA, TUCASA, AY, Pathfinder, Adventurer na kadhalika na kuendesha shughuli zihusianazo na vyama hivyo**

## SURA YA 7: WATEKELEZAJI WA UHAMASISHAJI WA ELIMU YA KIKRISTO

Ushirikiano wa mtu mmoja mmoja, idara na idara, kanisa na kanisa au mtaa na mtaa unahitajika sana ili kuboresha na kuitegemeza elimu ya kikristo katika makanisa yetu. Zifuatazo ni ngazi au makundi mbalimbali yanayohusika katika uhamasishaji wa wa elimu ya kikristo:

### i. Ngazi ya Kanisa Mahalia

- Katibu wa Elimu wa Kanisa kama mtendaji mkuu.
- Mchungaji au Mzee wa Kanisa kama Mratibu.
- Mratibu wa Huduma za Watoto mtendaji shirikishi.
- Mkurugenzi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo (VBS) – mtendaji shirikishi.
- Kiongozi wa Kaya na Familia – Mtendaji shirikishi

### ii. Ngazi ya Konferensi

- Uhamasishaji makanisani kwa kutumia vyama vya wanafunzi wa Sekondari na vyuoni (ASSA & TUCASA). Msimamizi ni Mkurugenzi wa Huduma za Chaplensia akisaidiana na Mkurugenzi wa Elimu.
- Uhamasishaji makanisani kwa kutumia watoto wa Chekechea wanaosoma katika Nursery schools na Day Care centres. Mratibu ni Mkurugenzi wa Elimu.
- Uhamasishaji makanisani kwa kutumia shule za kanisa zilizopo. Mratibu wa Elimu akitumia Wakuu wa Shule: Mfano; Bupandagila Adventist Primary School, Bupandagila Secondary School, Ngulyati Secondary School, Nyanza Adventist Secondary School n.k
- Uhamasishaji makanisani kwa kutumia shule za watu binafsi zinazondeshwa kikanisa. Mratibu ni Mkurugenzi wa Elimu akitumia Wakuu wa Shule/Wenye shule. Mfano: Geita Adventist Primary and Secondary School, Kusekwa Memorial Secondary School, Edden Valley Primary School.

## SURA YA 8: MKAKATI WA UHAMASISHAJI

**a. Kutumia matukio muhimu kanisani. Mfano:**

- Sabato ya 13, program ya Watoto
- Adventurer day
- Pathfinder Day
- Programu maalumu siku za Makambi
- Sabato ya watoto kanisani
- Wiki ya familia kanisani
- Mother's Day
- Wachungaji na wazee kuzungumzia umuhimu wa malezi wakati wa kuwaombea/kuwabariki watoto.

**b. Kutumia makanisa/Familia vielelezo**

- Makanisa yaliyo elewa mapema yatende, mengine yawaige.
- Ikibidi yachaguliwe makanisa yatakayotumika kama "makanisa vielelezo"
- Zitafutwe familia zitakazojitolea kutumiwa kama familia kielelezo zitakazoshirikiana kutoa malezi hayo.

**c. Kutumia watoto wenye karama/vipawa**

- Watoto wenye uwezo wa kuhutubu kwa lugha wanayomudu vema watambulike na kuadaliwa kwa kupewa masomo wanayopendelea
- Watoto hawa wazunguke makanisani kwa kutumia nafasi iliyopo (kwa kurejea kipengele c& a)

**d. Masomo maalumu yaandaliwe**

- Hotuba za afya na kiasi zinazotolewa na watoto(orations)
- Hotuba za kuelimisha uma juu ya madawa ya kulevya, UKIMWI, na ulevi wa pombe na uvutaji tumbaku na bangi.
- Hotuba za mtindo wa maisha kutahadhalisha watoto na vijana juu ya ubakaji, ulevi, matumizi ya mtanda isivyofaa: Mavazi yasiyo ya heshima yaepukwe; mwonekano usio na adabu wa kukaa uchi; na mapambo yasiyomsaidia mtu kuwa mzuri au kuwa mwema. (Modesty and Christian Grooming)
- Hotuba za shuhuda binafsi za visa vya maisha ya ushindi dhidi ya dhambi. (Kile Mungu alichomfanyia mtoto kama matokeo ya kujiweka chini ya ulinzi na uongozi wa Mungu)
- Udhihirisho wa maisha ya maombi na nguvu zipatikanazo kwa mtu anayemuomba Mungu sana. Shuhuda zitolewe zilizochaguliwa vizuri.

**e. Programu zinaweza kufanyikia mashuleni**

- Kipindi cha dini cha ratiba ya shule kinaweza kutumiwa kwa ruhusa na maelekezo ya mwalimu wa dini, aliyewekwa na kanisa
- Kipindi cha maombi ya Ijumaa jioni au Jumamosi mchana shuleni kiandaliwe vizuri na shule jirani ialikwe kuleta program; wanafunzi waalikwe kuja kushirikiana na wageni.
- Masharti zaidi yanakaribishwa ili kuongeza ubunifu na ufanisi.

## SURA YA 9: MWONGOZO WA KURUHUSIWA KUENDESHA SHULE KWA KUTUMIA JINA NA MFUMO WA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO

Uendeshaji wa Taasisi zenye kutoa huduma kwa jamii kama vile, shule au Hospitali, katika nchi nyingi, unatawaliwa na kuelekezwa na sheria za nchi. Kwa kuzingatia sheria hizo katika nchi mbali mbali, kanisa letu ambalo ndilo limesajiliwa kisheria, likitambulika kama mmiliki mkuu wa taasisi zilizo chini yake, limejiwekea sera za kudhibiti, kutawala na kuelekeza uendeshaji wa taasisi zake kwa kuzingatia Falsafa, Makusudi na Malengo yake ili kutimiza Utume wake ulimwenguni. Maelekezo yafuatayo yamekusudiwa kutumika kama mwongozo au sera za kuzingatiwa ili kuruhusiwa kuendesha shule/taasisi za elimu zinazotumia jina au mfumo wa kanisa, la Waadventista Wasabato.

**Mamlaka ya kanisa na Chimbuko lake**

"Kama Muumbaji, Mkombozi na Mruzuku, Bwana na Mfalme wa viumbe wote Mungu pekee ndiye chimbuko la mamlaka ya Kanisa. Alikasimu mamlaka kwa manabii na mitume wake (*2 Wakor. 10:8)*. Hivyo, walikuwa wanachukua fursa muhimu na ya aina ya pekee katika upelekaji wa Neno la Mungu na urekebishaji wa maadili ya Kanisa (*Waefeso 2:20), Mwongozo wa Kanisa, Toleo 18, uk. 27 -28)*

**Mamlaka ya Kanisa la Waadventista Wasabato leo ni sawa na mamlaka ya Kanisa wakati wa Mitume/Kanisa la Awali)**

Kwa kuzingatia jukumu kuu la utume wa Kanisa tangu zamani hadi siku hizi, ni wazi kwamba mamlaka ya Kanisa la Waadventista Wasabato leo ni sawa na mamlaka ya Kanisa la Awali (la Mitume). Kanisa la Awali, (sawa na kanisa la Waadventista Wasabato leo), lilikuwa na mamlaka ya kusuluhisha matatizo ya ushirika na kudhibiti kanuni zinazotawala kanisa. Usimamizi wa kichungaji, ufundishaji wa imani na kuhubiri yote yalidhibitiwa na kanuni zinazotawala kanisa. (*Mwongozo wa kanisa toleo la 18, uk. 28*).

Tofauti inayoonekana kuwepo ni katika mfumo wa Uongozi. Kanisa la Awali, Wazee na Maaskofu walikuwa na mamlaka makubwa (*Mwongozo wa Kanisa, Toleo la 18, uk. 28)* wakati Kanisa la Waadventista Wasabato mamlaka yamo katika mapenzi ya jamii ya watu, chombo kikuu kikuu chenye mamlaka kikiwa ni *Konferensi Kuu ulimwenguni* kupitia *Kamati kuu Tendaji ya konferensi* (**Mwongozo wa Kanisa, toleo la 18, uk. 28**).

Sera zinazotungwa na Konferensi Kuu ya Kanisa ulimwenguni ni za aina mbili ambazo ni:

i. Sera za kusimamia utume wa Kanisa, zinazoelekeza makanisa na taasisi zilizo chini ya Kanisa la Waadventista Wasabato, zimewekwa kwa pamoja katika kitabu kiitwacho "**Mwongozo wa Kanisa** au **Kanuzi za Kanisa** (jina la zamani)", kitabu kinachoweza kufanyiwa marekebisho, yanayoonekana kuwa ya lazima, kila baada ya miaka mitano ili kuongeza ufanisi.

ii. Sera za kusimamia utendaji wa Kanisa na taasisi zake kiulimwengu, kwa kuzingatia mahusiano na Sera zinazotawala nchi mbalimbali, hasa kuhusiana na ajira za watumishi au uendeshaji wa Kanisa. Sera hizo zote zimewekwa ndani ya kitabu kiitwacho: *Seventh-Day Adventist Church Working Policy (SDA WP).* Ndani ya kitabu hiki, kuna sera za utendaji wa kila idara na Taasisi ya Kanisa kuainisha falsafa, malengo, na Tamko la Utume wa Idara hiyo. Sehemu ya matamko hayo yamo ndani ya Mwongozo wa Kanisa. Ni muhimu kuyajua haya:

- Maelekezo ya kufanyia kazi kwa ngazi ya Kanisa mahalia yamo katika Mwongozo wa kanisa, Toleo la 18, uk 96 – 97.
- Mwongozo wa Kanisa unafunua kuwa kuna maelezo ya ziada yanayofafanua Sera za Elimu na mapendekezo ya Kanisa**.** (Mwongozo wa Kanisa Toleo la 18, uk 96-99) tena kwamba wale wasioamini na kuwa radhi kufuata hizo sera na mapendekezo ya Kanisa kuhusiana na Elimu ya Kikristo ilivyo, wasichaguliwe kuongoza shule kama wajumbe wa Bodi (uk 98).
- Sera zinazoelekeza na kuongoza uendeshaji wa Huduma za Idara ya Elimu zimo katika kitabu cha: ECD Working Policy ya 2004, uk. 203 – 224) maelezo yaitwayo: ECD Department of Education, FE 20 na FE 25, FE 30, FE 35, FE 40, FE 45, FE 50, FE 55, FE 60, FE 65, FE 70, FE 75, FE 85. Ni muhimu kuhakikisha maelekezo hayo kila shule inayo na inayazingatia.

**Kwa mujibu wa mfumo wa Elimu wa Kanisa la Waadventista Wasabato,** mambo **9** yafuatayo ni ya lazima kuwa bayana kabla shule yo yote kabla haijakubaliwa au haijatambulika kuwa iendeshwe chini ya mfumo unaotumia jina la Waadventista Wasabato.

i. Umiliki wa ardhi na wa majengo ya shule uko chini ya Misheni au Konferensi.
ii. Waalimu na wafanyakazi wengine ni Waadventista Wasabato wenye ushirika unaoeleweka na kujidhihirisha kwa vitendo.
iii. Waalimu wanaohitajika kiidadi na kisifa (ujuzi kitaaluma) wapo.
iv. Vifaa vya kufundishia ikiwemo Maktaba vipo na inatosheleza.
v. Uwezo wa kifedha, kujitegemeza kimahitaji upo na umedhihirishwa.
vi. Mtaala ulioandaliwa umetimiza malengo ya Elimu ya kikristo, Biblia ikiwa ni kiini cha Mtaala.
vii. Wanafunzi walio wengi wanatoka katika nyumba za kiadventista, wawe wamebatizwa au la.
viii. Wajumbe wa Bodi ya shule wote ni washiriki wa Kanisa.
ix. Mfumo na uendeshaji una msingi wake katika falsafa ya Kanisa la Waadventista, msisitizo ukiwa juu ya ubora wa kitaaluma.

**Mambo muhimu ya kuzingatia ili idhini itolewe kuanzisha au kuendesha shule ya awali au ya msingi**

i. Andiko la kuonyesha hitaji la kielimu la kulazimika kuwepo kwa shule hiyo hapo inapoombwa kuwepo.

ii. Kudhihirisha utoshelevu wa majengo na vifaa muhimu vihusikavyo na kuanzisha shule hiyo.
iii. Ushahidi wa kuthibitisha kuwa waombaji wanao uwezo wa kujiendesha kifedha.
iv. Mtaala utakaotumika kufundishia uwe umepata idhini ya Bodi ya Elimu ya Union/Koferensi.
v. Udhihirisho wa upatikanaji wa waalimu wa kutosha weye sifa za kitaaluma na uwezo wa kufundisha.
vi. Uwezo wa kutawala bajeti udhihirishwe.
vii. Kuonyesha mpango endelevu wa upatikanaji wa wanafunzi watakao changia upatikanaji wa fedha kukidhi uendeshaji wa programu.
viii. Mkuu wa shule, majukumu yake ya utawala na ufundishaji yaonyeshwe bayana.
ix. Idadi ya vipindi vya kila mwalimu ikubaliane na Sera za Bodi ya Elimu ya Union/Konferensi, aidha Wizara ya Elimu ya serikali.
x. Muda wa kila kipindi (ratiba ya vipindi) ipatane na sera za Bodi ya Elimu ya Union/Konference, aidha Wizara ya Elimu ya serikali.
xi. Kuonyesha sera zao walizo nazo, zinazopatana na sera za Idara ya Elimu ya Misheni/Konferensi kuelekeza maswala ya: Utawala na Uongozi, Fedha, Mtaala, na Utumishi.

**Shule Zinazoendeshwa Kikanisa**

Shule zinazoendeshwa na kikanisa ni za aina nne:

i. Zilizojengwa na zinazofadhiliwa na oganizesheni ya kanisa iliyoijenga, iwe ni kanisa mahalia au umoja wa makanisa, au taasisi nyingineyo, (Church School).
ii. Zilizojengwa na serikali na kuendeshwa na ufadhili wa serikali na kanisa, (Community Church School);
iii. Zilizojengwa na kufadhiliwa na serikali, kanisa likishirikishwa katika uendeshaji, (Grant-aided School).
iv. Shule za nyumbani, kwa ajili ya wanafunzi wa watumishi wa kimataifa waliokosa mfumo wa kikanisa pale walipo, (Home school or directed schools) Je shule aina gani ni shule unayotafuta kuanzisha?

**Shule za watu binafsi** au makundi ya watu binafsi, walio Waadventista Wasabato, wanaoendesha shule zao kwa mfumo wa kiadventista, lakini wenye mtazamo wa kibiashara, wao ni tofauti na shule zinazoendeshwa na Kanisa. Hawaruhusiwi kutumia ardhi ya Kanisa. Shule za jinsi hii zinapohitaji kutambulika na Kanisa au kushirikiana na Kanisa zinaomba idhini ya kutambulika hivyo.

Kuna mambo ya msingi yahusianayo na program ya shule ambayo kila taasisi inayotaka kuendesha shule inawajibika kuyaandaa/kuyaweka sawa/kuyatunza.

i. Andiko la Mradi unaokusudiwa kufanywa, huandaliwa na kutumwa Union/Divisheni angalau miaka miwili kabla ya shule kuidhishwa/kufanyiwa ukaguzi wa awali na ngazi hizo ndipo ianze.
ii. Ombi la kujenga shule, na idhini iliyotolewa na Serikali.
iii. Ombi la kumiliki na kuendesha shule, na idhini iliyotolewa na serikali.

iv. Ombi la usajili wa shule, na cheti cha usajili wa shule.
v. Ndani ya Andiko la Mradi yafuatayo yanakuwa bayana:

- Ni taasisi gani ya elimu inayokusudiwa, kati ya: Awali, Msingi, Sekondari, Chuo? Bweni au Kutwa? Wavulana au Wasichana? Ya kawaida au Maalumu?
- Kwa nini shule hiyo iwepo? (Falsafa, Makusudi na Malengo, kuonyesha maelezo yakinishi kutetea hoja).
- Idadi ya wanafunzi wanaoianzisha na wanaotegemewa kuijaza.
- Programu ya Elimu itakavyokuwa.
- Master plan ya eneo la shule (Mkakati wa ujenzi na maendeleo ya shule)
- Master plan ya kiroho (Mambo ya kihoro yatakayofundishwa na jinsi yatakavyofundidhwa).
- Waalimu wanaohitajika na watakavyo patikana.
- Fedha za kuendeshea shule zinazohitajika na jinsi zitakavyopatikana.

vi. Sera za uendeshaji wa Mradi kuonyesha

- Upatikanajiwa Watumishi na utumishi wao (Ajira na mikataba).
- Utunzaji wa mali za Mradi.
- Mfumo wa Uongozi na usimamizi.
- Majukumu ya kila ngazi katika mfumo uliopendekezwa

vii. Utunzaji wa kumbukumbu muhimu

Miongoni mwa nyaraka muhimu za kuhifadhiwa vizuri na zenye rekodi sahihi ni zifuatazo:

- ***"School Logbook"*** Ina kumbukumbu ya waliotembelea shule hiyo tangu inajengwa hadi siku ya jana yake jioni, watu wenye malengo ya kutoa huduma kwa shule.
- ***"Admission Register"*** Inatunza kila jina la mwanafunzi aliye wahi kusoma hapo shuleni, kuonyesha mwaka alioingia, namba ya usajili, jinsi alivyoingia na mwaka na jinsi alivyotoka.
- ***"School Baraza"*** Ina tunza muhtasari (minutes) wa ajenda muhimu na maazimio muhimu yaliyofanywa hadharani katika kikao kilichohusisha waalimu wote, wafanyakazi wote, na wanafunzi, kinachofanyika angalao mara mbili kwa muhula, mwanzoni mwake, na mwishoni mwake.
- ***"Staff Meeting/Teachers Meeting Minutes"*** Ni miniti zinazotunzwa zinazoonyesha mahudhurio na ajenda zilizojadiliwa, aidha na kikao cha Waalimu kama sehemu ya uboreshaji wa ufanisi wa maendeleo ya shule kitaaluma.
- **"*Workers Meeting Minutes"*** Ni miniti zinazotunzwa, kuhifadhi mahudhurio na maazimio yatokanayo na mikutano ya watendakazi wote, waalimu na wasio waalimu, kama sehemu ya ushirikishwaji wa kiuongozi katika kutatua baadhi ya masuala yanayohitaji kundi hili, iwe ni kiusalama, au kinidhamu, au kiustawi wa jamii.
- ***"Schoool Discipline Record"*** Ni muhtasari unaotunzwa kuhifadhi kumbukumbu za vikao vyote ya nidhamu vilivyokaa, na hatua

zilizochukuliwa kama matokeo ya makosa yaliyo sababisha Kamati ya nidhamu iitishwe.

- **"School Handbook"** Ni mwongozo unaoelekeza haiba ya jumuia ya shule ilivyo. Ndani humo kuna sheria za shule, taratibu za kuishi shuleni, mipaka ya kimahusiano, kile shule inachotetea sana (falsafa na malengo); Maelezo kuhusu waalimu na wafanyakazi n.k.

Kwa kawaida, kumbukumbu hizi zote hutunzwa na Makamu mkuu wa Shule, au na Mkuu wa shule pale inapobidi, nazo hazitakiwi kukosekana wakati wa Ukaguzi au zinapohitajika kwa rejea na uongozi ulio juu ya shule.
Bodi ya Elimu ya Kanisa la Waadventista ya Union/Konferensi inapofanya ukaguzi wa awali wenye nia ya kuisajili shule katika umoja wa shule zinazoendeshwa chini ya mfumo wa Kanisa, mambo haya yote huzingatiwa. Sasa jiulize na ujijibu swali hili muhimu. Je, wewe unayependa kutambulika kama shule mojawapo chini ya Kanisa la Waadventista Wasabato, je uko tayari kwa ukaguzi wa awali? Kama uko tayari, andika maombi ya kukaguliwa. Mwandikie mkurugenzi wa Elimu ambaye ndiye katibu wa bodi ya Elimu ya konferensi kwa anuani;

**Katibu wa Bodi,**
**Bodi ya Elimu ya Konferensi,**
**Kanisa la Waadventista Wasabato,**
**Konferensi ya Nyanza kusini**
**S.L.P. 401, MWANZA.**

## SURA YA 10: SHUGHULI ZA KATIBU WA ELIMU WA KANISA MAHALIA/KUNDI

### Kuchanguliwa kwa Katibu wa Elimu Wa Kanisa

Katibu wa Elimu au karani wa idara ya Elimu kanisani huchaguliwa na kanisa lake wakati wa uchaguzi wa mwaka unapofanywa.

### Sifa za Katibu wa Elimu Kanisani


i. Awe mshiriki wa kanisa la Wasabato aliyebatizwa anayeaminika, akisimamia vema imani yake na akiwa na sifa njema kanisani.
ii. Ajue na kuelewa misingi ya mafundisho yetu makuu 28 ya imani ya kanisa la Waadventista wasabato.
iii. Aelewaye misingi na umuhimu wa Elimu ya Kikristo na pia apendaye jinsi mipangilio hii inavyoendeshwa katika mashule ya Kisabato.
iv. Pangependeza zaidi yeye awe mwalimu aliyejitoa wakfu kwa kazi ya ualimu au awe kiongozi wa Elimu kama mwalimu mkuu wa shule au kiongozi yeyote wa elimu.

### Majukumu ya Katibu/Karani wa Elimu Kanisani

i. Kutembelea nyumba zote za wasabato ambapo pana watoto na vijana wa umri wa shule na kuwahamasisha wajiunge na shule zetu za primay na sekondari pamoja na vyuo vyetu vya ualimu na vyuo vikuu vya kisabato popote nchini.
ii. Kuwatembelea washiriki wasio na watoto wa umri wa shule na kuwahamasisha kutoa mchango wa fedha kusaidia shule zetu za kisabato na kuwasaidia pia watoto wetu maskini wasiojiweza wasomao katika shule zetu za kisabato.
iii. Daima kudumisha mawasiliano na wanafunzi wanaopenda mipangilio au taratibu au mafundisho ya kanisa letu la Kisabato.
iv. Kutayarisha programs kamilifu za kielimu inayodumu na ipendezayo makanisani.
v. Kusaidia wanafunzi waliomo kanisani wapate njia nzuri zaidi ya kushuhudia injili kwa vijana wenzao pamoja na walimu walio katika shule zisizo za Kiaadventista.
vi. Kujaribu kwa njia zozote zile kuhimiza kanisa letu kutoa Elimu ya Kikristo katika sehemu ambapo shule zetu za kisabato hazipo kwa kuhamasisha ujenzi wa chekechea, primary schools, sekondari, n.k.
vii. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamejumuishwa kimatendo kikamilifu katika shughuli zote na mipangilio yote na mafundisho yote ya kikanisa.
viii. Kutunza kila mwaka idadi ya watoto wote na vijana waliopo kanisani.
ix. Kuratibu ufundishaji wa vipindi vya dini mashuleni (katika shule za msingi na sekondari zillizo jirani na kanisa) chini ya usimamizi wa kamati ya elimu kanisani.

**Mapendekezo ya Division**

Katibu wa Elimu wa kanisa awe mwana baraza la kanisa lake na pia awe katika kamati ya bodi ya shule ya kanisa. Iwapo shule moja inaendeshwa na makanisa kadhaa, kila katibu wa Elimu wa makanisa hayo awe mshiriki katika kamati ya bodi ya shule hiyo kwa kupeana zamu.




**Note 5: Ingependeza zaidi kama katibu wa elimu akiwa mwalimu aliyejitoa wakfu kwa kazi ya ualimu au awe kiongozi wa Elimu kama mwalimu mkuu wa shule au kiongozi yeyote wa elimu**.

## SURA YA 11: UINJILISTI KUPITIA ELIMU

Uinjilisti kupitia elimu hufanyika ndani na nje ya kanisa. Hulea watoto au washiriki waliomo ndani ya kanisa na kuwatafuta kondoo walio nje ya zizi la Bwana yaani humlea mwana mkubwa na kumrejesha mwanampotevu. Kufuatia utume katika elimu ndani ya kanisa la Waadventista wa Sabato, hakika hakuna mtoto aliyeachwa nyuma (No Child is Left Behind -NCLB)

### Faida Za Kuanzisha Shule Katika Kanisa Mahalia

Neno la Mungu linasema**, "*Yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu, yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa Kama utepe katikati ya macho yenu, nayo wafunzeni vijana wenu Kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, Na utembeapo njiani, na ulalapo na uondokapo" (Kumb: 11:18-19).***

Mungu anatuhimiza kuwaambia watoto wetu neno lake tuketipo katika nyumba zetu na tutembeapo njiani na tulalapo na tuondokapo. Kwa maneno mengine, tuna wajibu wa kuwafundisha watoto wetu wakati wote. Kama hivyo ndivyo, Je, ni kwa namna gani watoto hawa wanaweza kuambiwa neno la Mungu, ikizingatiwa kuwa wanakuwa hawako pamoja na wazazi kwa muda mrefu wanapokuwa masomoni hususani katika shule za bweni? Hakika hii ni changamoto kubwa na tusipoangalia watoto wetu wanaweza kukosa fursa ya kuambiwa Neno la Mungu kwa sababu tu ya kuwa masomoni.

Hata sasa ni wakati wa makambi, jiulize ni watoto wangapi wapo kambini wakati shule zimeshafunguliwa? Katika mazingira haya, shule za kanisa zinaweza kuwa suluhisho kwa changamoto hii. Katika shule za kanisa za kutwa na za bweni kwa kuwa Neno la Mungu hutolewa kwa watoto wetu wawapo shuleni kwa kuwa ni sehemu ya elimu ya kiadventista.
Shule za kanisa ni sehemu ya kupanda mbegu ya neno la Mungu kwa ufanisi kuliko hata mikutano ya injili inayoendeshwa na makanisa.

Mbegu hizi huweza kumea, kukua na na kuzaa matunda. Kwa kutambua hilo Ellen G. White alisisitiza sana makanisa mahalia kujenga shule. **"*Siyo kwamba nyumba ya ibada pekee ndiyo ijengwe, lakini mipango yote ya lazima ifanywe kwa kuanzisha shule ya kudumu (Testimonies for the Church, volume 6, uk. 108). "Shule pia yahitajika ambapo mafunzo ya Biblia yatatolewa kwa watoto. Chumba cha darasa chahitajika sawa kabisa kama jengo la kanisa" (Testimonies for the Church, volume 6, uk. 109).***

**Zifuatazo ni baadhi ya faida za kuwa na shule katika kanisa mahalia:-**

i. Watoto wengi wataweza kupata elimu ya kikristo katika maeneo yao na hivyo kusaidia kukabiliana na changamoto zinazofanya watoto wengi wa washiriki na wa wasio washiriki wa kanisa wasisome katika shule za kanisa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na shule kuwa mbali, ukosefu wa nafasi katika shule zetu kwa sababu shule ni chache, ada

kubwa na baadhi wazazi kutopenda kuwapeleka watoto wao katika shule za bweni.

ii. Watoto na vijana wa kanisa watajengwa katika msingi bora wa imani wakiwa na umri mdogo na itakuwa si rahisi kwa shetani kuwateka. Kwa mujibu wa **ELLEN G WHITE"** ***Mungu amelichagua kanisa kuwa mlinzi ili liwatunze kwa uangalifu mkubwa vijana na watoto na kushika doria ili kuwaona maadui wanapokaribia na kutoa tahadhari dhidi ya hatari" (Counsels to Parents, Teachers and Students, uk .165).***

iii. Kwa kuwa shule itakuwa inapokea wanafunzi wa dini zote na hata wasio na dini, kanisa litatumia shule kama uwanja wa mahubiri ambapo wanafunzi wa dini zote watapata fursa ya kufundishwa neno la Mungu na kupitia mafundisho hayo wanaweza kutoa maisha yao kwa Yesu. Kupitia shule, watu wanaweza kupata ujumbe wa neno la Mungu kwa fedha zao wenyewe badala ya sisi kutumia fedha zetu kuwahubiri ujumbe huo kama tunavyofanya kwenye mikutano ya injili (effort).

iv. Kupitia shule, injili ya Yesu inaweza kupenya hata katika maeneo ambako si rahisi wahubiri kufika. Kutokana na mvuto chanya wa watoto wanaosoma katika shule za kanisa, wazazi, ndugu jamaa na marafiki wa watoto hao wanaweza kuguswa na kuamua kumfuata Yesu. Vipo visa kadhaa ambapo watoto waliosoma katika shule za kanisa, kwa mvuto wao, waliweza kusababisha wazazi wao na watu wengine wa karibu kumpokea Yesu. Waweza kuhakikisha hili kupitia utafiti mdogo tu ambao unaonyesha idadi kubwa ya washiriki katika kanisa letu hivi leo wametoka katika maeneo ambako pana shule za kanisa nyingi ambako ndipo wamisionari walisimika mizizi ya injili. "***Yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu, yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu, nayo wafunzeni vijana wenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na njiani, na ulalapo na uondokapo" (Kumb: 11: 18 - 19).***


v. Shule zitasaidia kupata washiriki walioiva vizuri. Watoto wanaolelewa katika maadili ya kanisa kwa muda wa miaka saba au minne ya masomo yao ni tofauti kabisa na waumini wanaobatizwa katika effort ya wiki mbili au tatu na baada ya hapo wanaachwa bila malezi ya kiroho ya karibu. Hivi sasa kanisa letu linakabiliwa na changamoto ya malezi ya kiroho kwa waumini wapya. Tunabatiza watu wengi sana katika mikutano yetu ya injili, lakini ukifanya tathmini baada ya muda fulani, ni wachache sana wanabaki kanisani na kuendelea kuwa washiriki waaminifu. Wengi wanarudi nyuma kutokana na malezi duni ya kiroho. Wale wanaobatizwa wakiwa katika shule za kanisa huendelea kupata malezi na mafundisho ya kiroho kwa ukaribu sana na hivyo hukomaa na kuwa washiriki imara na wengi wao wamedumu kuwa washiriki waaminifu katika maisha yao yote.

vi. Shule za zitasaidia kuwaweka watoto pamoja ili waweze kujenga mahusiano mazuri na ya muda mrefu baina yao. Wanafunzi hujifunza mengi kutoka kwa wanafunzi wenzao kupitia nguvu ya makundi rika (peer pressure) pengine kuliko hata wanavyojifunza kutoka kwa wazazi

na walimu wao. Kwa sababu hiyo ni vizuri kuwaweka katika mazingira yatakayokuza maadili yao kutokana na nguvu hii ya makundi rika katika shule za kanisa. Zaidi ya kujifunza kutoka kwa wanafunzi wenzao, mvuto wa wazazi na walimu wacha Mungu wanaofundisha katika shule za kanisa ni somo zuri sana kwa watoto. Somo hili litaeleweka vizuri zaidi ikiwa litafundishwa nyumbani, shuleni na kanisani. Ikiwa somo hili litafundishwa nyumbani tu na kidogo kanisani halafu shuleni anakutana na walimu wasiomjua Mungu na kupata somo tofauti, ni dhahiri kuwa mtoto atapata masomo yanayokinzana na atachanganyikiwa asijue kipi afuate.

vii. Shule za kanisa zitawaepusha watoto waadventista na changamoto za kuvunja Sabato zinazowakabili wanafunzi wanaosoma katika shule zisizo za kiadventista ambako baadhi ya shughuli za masomo na zisizo za masomo hupangwa kufanyika siku ya Sabato. Baadhi ya shughuli hizo ni masomo ya ziada, michezo, mitihani, sherehe za shule, usafi wa mazingira n.k. Wengi wa watoto waadventista wamejikuta wakianguka katika imani yao kwa sababu ya changamoto hizi. Suluhisho la changamoto hizi ni kuwa na shule zetu ambazo zinaheshimu maelekezo ya neno la Mungu.

viii. Utafiti umeonyesha kuwa *jinsi mtoto anavyotumia muda mrefu akipokea elimu ya kiadventista ndivyo anavyoelekea kulipenda, kulitumikia na kulitegemeza zaidi kanisa*. Kinyume chake pia ni kweli; baadhi ya waumini wetu waliosoma katika taasisi za elimu zisizo za kiadventista wamekosa hamu ya kulitumikia kanisa kutokana na mvuto hasi wanaoupata katika shule na vyuo wanakosoma.




*Chati hii inaonyesha utafiti uliofanywa katika kanisa la Waadventista wa Sabato na kutolewa taarifa kupitia idara ya Elimu ya katika Halmashauri kuu ya Kanisa (2012/2013). Utafiti unaonyesha asilimia za uwezekano wa kulipenda kanisa na*

*kulitegemeza ikiwa mtoto hakupata elimu yoyote ya Kiadventista- 45%, Elimu nyumbani pekee yake 64%, Elimu nyumbani na katika kanisa mahalia -84%, na ikiwa amepitia elimu nyumbani, katika kanisa mahalia na shule za kanisa ni– 88%.*

ix. Shule za kanisa zitasaidia kupanuka kwa kanisa letu. Historia inaonyesha wazi kuwa katika sehemu ambazo kanisa lilijenga shule, waumini wengi walipatikana na kanisa likapanuka kwa kasi kubwa. Japo hatuna takwimu za mgawanyiko wa washiriki kimakabila hapa nchini lakini ukweli ni kwamba waadventista wasabato wengi wanatoka katika makabila ya Wapare, makabila ya mkoa wa Mara (Wajita, Wakurya, Wajaluo na wengineo), Wasukuma, Wanyakyusa na Waha. Sababu kubwa ni kwamba wamisionari walipoleta injili katika maeneo hayo walijenga shule pia. Historia inaonyesha kuwa, hadi kufikia mwaka 1963, kulikuwa na shule za msingi za Kiadventista zipatazo **192** hapa nchini. Kati ya hizo 46 zilikuwa katika milima ya Upare na Usambara, 48 zilikuwa Usukumani, 90 mkoa wa Mara (Majita na Utimbaru), 7 zilikuwa mkoa wa Mbeya na mkoa wa Kigoma kulikuwa na shule moja. Bila shaka umepata jibu, ikiwa huwa unajiuliza kwa nini washiriki wengi wa kanisa letu wana asili ya makabila yaliyotajwa hapo juu na kwa nini kuna waumini wachache sana wenye asilia ya mikoa kama vile Singida, Dodoma, Tabora, Morogoro, Rukwa, Ruvuma na mikoa yote iliyo katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi. **Kama tunataka kupata waumini wenye asili ya mikoa hiyo basi tujenge shule katika makanisa mahalia yaliyoko katika mikoa hiyo**. Tumeitwa kupeleka injili katika kila taifa, kabila, lugha na jamaa (**Ufunuo 14:6**). Kama tunaishi na watu wa kabila fulani na hawamjui Mungu, basi hatujatimiza wajibu wetu. Kumbuka sote tu wa zizi moja na Bwana wetu ni mmoja.

## SURA YA 12: NINI KIFANYIKE ILI KUBORESHA ELIMU YA KIADVENTISTA KATIKA MAKANISA YASIYO NA SHULE?

Neno la Mungu linasema, ***"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17: 3)***. Elimu ya kiadventista inaitambulisha Biblia kama msingi wa kufikiri na kutathmini mambo. Elimu hii huwaandaa watu kumfahamu Mungu pamoja na Yesu Kristo aliyemtuma kutukomboa dhambini. Kanisa mahalia lina fursa nzuri kuwafundisha watoto na vijana kumfahamu Mungu na Yesu kama mwokozi wa maisha yao. Kabla ya kufikia umri wa kwenda shule au pale ambapo haiwezekani kuendesha shule ya kanisa, kanisa mahalia linapaswa kuandaa programu za mafundisho ya Biblia na malezi ya Kikristo kwa watoto na vijana ambayo wenzao huyapata katika shule za kanisa. Kwa bahati nzuri, kanisa letu lina programu nzuri kupitia idara za vijana, watoto, shule ya Sabato n.k. ambazo zikitumiwa vizuri zinaweza kuwapatia elimu ya kweli inayowaelekeza katika uzima wa milele.

Katika makanisa mengi elimu ya kiadventista haijapewa kipaumbele. Utakuta katika makanisa hayo hakuna mhubiri kwa ajili ya watoto wakati wa ibada kuu. Mara nyingi, mhubiri wa watu wazima huachiwa kuamua ama atoe somo la watoto au atoe somo la watu wazima tu. Na pale panapokuwa na mhubiri wa watoto, ni mara chache sana kukuta Mchungaji au Mzee wa Kanisa anahubiri watoto. Wahubiri wanaopangwa ni wale ambao huwa hawapangwi katika ibada kuu ya watu wazima. Watoto wamegeuzwa kuwa sehemu ya kujifunzia kuhubiri au kufundisha kabla ya mtu hajaaminiwa na kanisa kwa ajili ya kuhubiri au kufundisha watu wazima! Na hata wakati mwingine kile kinachohubiriwa kwa watoto hutolewa bila maandalizi na hivyo kuwa kama kutimiza wajibu tu. Kama kuna mahali unaweza kujishusha au kujidhalilisha utu wako ni pale unapofundisha bila maandalizi ya kutosha kwa watoto, wanakudharau na kupoteza imani na wewe siku zote. Linda hadhi yako kwa kufanya yaliyo mema na yanayokubalika kwa watoto na utakuwa mtu wa kuigwa katika maisha yao yote. Ikiwa waigizaji wa kidunia wanajiandaa vizuri ili kukuvutia na wakati wafundishacho siyo halisi, kwa nini wewe ufundishaye kitu halisi usijiandae vizuri ili uache mguso halisi kwa watoto?

Jambo jingine la kusikitisha ni kuwa, makanisa mengi hayafikirii kuandaa mazingira mazuri kwa ajili ya watoto kufurahia ibada na programu zingine za watoto. Majengo au sehemu wanazofanyia ibada huwa ni chafu au zina vumbi, hawana viti vya kukalia na hivyo hukaa chini kwenye vumbi au jua kali wakati wazazi wao wamekaa sehemu nzuri kanisani. Kwa wale walio na majengo ya ibada kwa ajili ya watoto mara nyingi huwezi ukasikia kwaya imeenda kuimba huko wakati wa ibada ya watoto. Je, huko anayeabudiwa ni tofauti na anayeabudiwa kwa watu wazima? Ikiwa zote ni ibada, kwa nini zisipewe heshima sawa?

### Nini kifanyike?

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ya kuboresha elimu ya kiadventista katika kanisa mahalia:

- Makanisa yasipuuzie mafundisho ya vijana katika umri mbalimbali (Wavumbuzi, mabalozi, Watafuta njia na vijana wakubwa). Mchungaji na wazee wa kanisa wahakikishe Idara ya Huduma za vijana na ile ya Huduma za Watoto zinakuwa hai wakati wote.
- Vijana wahusishwe katika nyanja zote za uongozi wa kanisa. Kwa mfano, vijana wakichaguliwa kuwa wazee wa Kanisa au mashemasi wanaweza kufanya kazi pamoja na moafisa wazoefu na kujifunza kutoka kwao.
- Watu wenye uwezo na karama ya kufundisha au kuhubiri watoto ndio wapangwe au wachaguliwe kufanya hivyo. Tusipange au kuchagua wahubiri na walimu wa watoto ili kujaza ratiba au kukamilisha tu idadi ya walimu. Kuhubiri au kufundisha watoto na vijana kunahitaji karama au mafunzo maalum. Kanisa liangalie uwezekano wa kuandaa mafunzo/semina maalum kwa ajili ya walimu na wahubiri wa watoto.
- Pale inapowezekana, kuwe na jengo la watoto kwa ajili ya ibada na programu zao. Si haki kabisa kuwapeleka watoto nje wakati wa shule ya Sabato au programu zingine ambako wanaweza kupigwa baridi, jua, vumbi n.k huku wazazi tukibaki kanisani. Kama kweli tunawapenda watoto wetu ni bora tukae nao kanisani au watu wazima tuende nje ili watoto wakae katika mazingira mazuri ndani ya kanisa.
- Wakati wa uchaguzi wa kanisa, tuchague viongozi wa idara za huduma za watoto na idara za vijana wenye karama ya kuhudumia watoto na vijana.
- Wazazi wasiwakataze watoto na vijana wao kuhudhuria mafundisho na programu za watoto na vijana. Vilevile watoto na vijana wanunuliwe vitabu vinavyowahusu kama vile lesoni, vitabu vingine na vifaa vinavyohitajika kama vile sare za vyama pamoja na kulipia gharama za ushiriki wao katika mikutano na makambi ya vijana.
- Ibada za watoto na watu wazima zipewe hadhi sawa kwa maana ya upangaji wa wahudumu na mhubiri anayepangwa ajiandae kikamilifu.
- Kwaya ya watoto ni njia nzuri ya malezi ya kiroho. Kila Kanisa liwe na kwaya hai ya watoto.
- Kina mama wajawazito na wale wanyonyeshao washirikiane na waalimu wa watoto kuandaa mazingira ya kiroho katika kanisa la watoto. Tuache kasumba ya kulifanya kanisa la watoto kama mahali pa kupeana habari za juma zima, tunaharibu mazingira ya kujifunzia neno la Mungu.
- Mjumbe wa Mungu (EG White) anasema kuwa, *shule zijengwe kokote ambako kazi imeanzishwa. 6T 108 kwani “kama watu wangehimiza kanisa wanamoshiriki kuanzisha shule ndogondogo zenye majengo kawaida yasiyo ya fahari kwa ajili ya kumtumikia Mungu, wangeweza kuwashikilia watoto wao katika mipaka yao. Australiasian Union Conference Record 26/July/1899 uk.3*
- Popote ambapo kuna makundi na makanisa yetu shule zijengwe kwa ajili ya watoto. *Advocate, June 10, 1902 uk.12.* Ellen White anasema, *jumla ya watoto sita na Zaidi watosha kujenga shule.6T 199.*
- Andaa kamati ya Elimu kanisani kwako ili kusimamia masuala yote ya elimu kwa kufuata taratibu.

**Mfumo wa Kamati ya Elimu katika kanisa mahalia**

Pamoja na ukweli kwamba mwongozo wa kanisa hauko wazi sana juu ya muudo wa kamati ya elimu sawa na kama ilivyo kwa idara zingine ndani ya kanisa, bado kanisa halikuwaacha ukiwa walengwa wa uhamasishaji wa elimu ya Kiadventista. Bodi ya elimu iliyokaa tarehe 11 mwezi Mei, 2000 katika iliyokuwa inaitwa Tanzania Union, Arusha ilipitisha maazimio yafuatayo kwa kura ya pamoja: "Kwa vile karani au mkurugenzi wa Elimu kanisani ana majukumu makubwa na mazito ya kuhamasisha elimu ya kikristo makanisani na kwa vile kitabu cha kanuni cha kanisa la Waadventista wa Sabato hakikuweka wazi muundo wa kamati ya Elimu ambao ungekidhi hitaji kubwa, imepitishwa rasmi kuwa kila kanisa liunde kamati ya Elimu ikiwa na wajumbe wafuatao:

i. Katibu wa Elimu kanisani (Mwenyekiti)
ii. Mzee wa kanisa anayesimamia idara ya Elimu (Mshauri)
iii. Viongozi wa vilabu vya vijana (AC, PF na Mabalozi)
iv. Kiongozi wa idara ya Huduma binafsi kanisani
v. Kiongozi wa Idara ya Huduma za Wanawake
vi. Kiongozi wa Uwakili kanisani
vii. Kiongozi wa Idara ya Huduma za Watoto
viii. Mhazini wa kanisa

Ilishauriwa kuwa kamati hii inapaswa kukutana kila Jumapili ya mwisho wa mwezi kwa ajili ya kujadili na kupanga mambo mbalimbali yahusuyo elimu.



**Note 6: Elimu ya kiadventista inaitambulisha Biblia kama msingi wa kufikiri na kutathmini mambo.**

## SURA YA 13: TARATIBU ZA KUANZISHA NA KUSAJILI SHULE

Shule ni kusanyiko, taasisi, Jumuiya au mahali kwa vyo vyote patakavyoitwa ambapo inatolewa elimu ya watu wazima kwa sekondari, elimu ya ualimu au elimu ya watu wazima kwa watu saba au zaidi kwa wakati mmoja, au vinginevyo na ikiwa mafunzo hayo yanatolewa moja kwa moja au kwa njia ya Posta, basi itamaanisha mahali ambapo mafunzo yanatayarishwa au mahali ambapo kazi za wanafunzi zinapokelwa zinatumwa au zinasahihishwa. Uanzishaji na usajili wa Shule na Walimu ni mojawapo ya majukumu yanayofanywa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi ili kuhakikisha kuwa Elimu inayotolewa kwa wadau inazingatia sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995. Sheria ya Elimu ya 25 ya mwaka 1978 na rekebisho la Na 10 la mwaka 1995.

### Aina za Shule na Maana zake

“**Shule ya Awali”** ni shule inayotoa elimu ya awali lakini endapo inatoa Elimu ya Awali, Msingi Sekondari au Elimu ya Ualimu, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu. Shule ya awali itamaanisha kuwa ni ile inayotoa Elimu ya Awali.

“**Shule ya Msingi”** ni shule inayotoa elimu lakini endapo shule inatoa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa mujibu wa Sheria ya Elimu, Shule ya Msingi ni sehemu ya shule kutoa Elimu ya Msingi.

“**Shule ya Sekondari”** ni Shule inayotoa Elimu ya Sekondari lakini endapo Shule inatoa Elimu ya Sekondari, Msingi, awali na Sekondari ni ile inayotoa Elimu ya Sekondari.

**“Taasisi ya Dini”** ni Taasisi yo yote inayoendeshwa na jumuiya ya kidini kwa makusudi ya kuwaandaa watumishi wa dini husika inayoendeshwa baada ya kupatiwa leseni na waziri.
“Shule ya mafunzo ya dini (Seminari)” ni mkusanyiko wowote, taasisi, jumuiya au mahali ambapo waziri ameridhika kuwa madhumuni yake au lengo kuu ni kutoa mafunzo ya dini.

### Uendeshaji wa Shule

“Meneja” katika mtazamo wa shule ni mtu anayehusika na uendeshaji wa shule au anayesimamia shughuli za wanafunzi shuleni, kupokea karo, kusimamia amfunzo kwa nji ya posta na mawasiliano ya ana kwa ana.
Ili kuanzisha na kusajili Shule yenye ubora unaostahili wadau hawana budi kufuata hatua mbalimbali kama zilivyoainishwa kwa kina katika Mwongozo wa Usajili wa Shule wa mwaka 1982”. Kwa kifupi hatua hizo ni kama zifuatazo:

Hatua ya Kwanza: Kibali cha Kujenga Shule

Mwenye nia na uwezo wa kuanzisha Shule atume maombi ya kutaka kujenga shule kwa maandishi kwa Kamishna wa Elimu. Maombi haya yapitishwe kwa Afisa

Elimu Wilaya itakapojengwa na Afisa Elimu Mkoa yakiwa na viambatanisho vifuatavyo:

i. Rejea mwongozo wa andiko la Mradi la Wizara.
ii. Bank Statement yenye zaidi ya Shilingi Milioni Sitini na mbili (Tshs. 62,000,000/=).
iii. Nakala ya hati/offer/uthibitisho wa kumiliki aridhi iliyotolewa kwa matumizi ya Shule inayotambulika kisheria na Serikali Kuu ya mtaa na Kijiji (eneo lisipungue ekari 7 na nusu Kijijini na 3 na nusu Mjini).
iv. Michoro ya Majengo ya Shule inayoonesha vipimo kwa kuzingatia viwango vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
v. Ramani ya Shule inayoonesha mpangilio wa majengo na viwanja vya michezo (site Plan).
vi. Cheti cha usajili wa kampuni/shirika/umoja/NGO iwapo shule ni ya Jumiya na Katiba yake au Mkataba wa Maridhiano (Memorandum of understanding or Articles of Association/Partnership deed)
vii. Endapo mdau anataka kutumia jina la mtakatifu(St.) awasilishe kibali kutoka kwa Askofu wa dhehebu la dini inayotambulika kinachoidhinisha matumizi ya jina hilo.
viii. Kamishna wa Elimu akiridhika na maombi hayo atatoa kibali cha kujengwa Shule kimaandishi, ndipo ujenzi utaanza.

Hatua ya pili: Kuthibitishwa kuwa Mwenye Shule na Meneja wa shule

Hatua hii ni kwa wale tu waliokamilisha hatua ya kwanza na inahusisha yafuatayo:

i. Mwombaji ajaze fomu Na. **RS. 6** ya kuomba kuthibitishwa kuwa Mwenye Shule na **RS. 7** ya kuomba kuthibitishwa kuwa Meneja wa Shule. Hatua hii itafanywa baada ya mwombaji kuwa amekamilisha ujenzi wa majengo yote muhimu kwa asilimia **75.**
ii. Majengo hayo ni lazima yawe yamekaguliwa na mamlaka za wilaya ambao ni: Mhandisi wa majengo, Afisa Afya na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Wilaya na kwamba fomu hizo ziwe zimepitishwa na Afisa Elimu wa Wilaya, Afisa Elimu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa.
iii. Wizara ikiridhika itatoa kibali cha maandishi cha kumthibitisha **Mwenye Shule** na **Meneja wa Shule.**

Hatua ya Tatu: Maombi ya Kusajili Shule

Hatua hii ni kwa wale tu waliokamilisha hatua ya kwanza na ya pili.

i. Mwenye Shule hujaza fomu na RS.8 ya maombi ya kusajili Shule baada ya kuwa amekamilisha mahitaji yote yanayotakiwa kwa Shule ya aina anayoiomba ambayo ni Majengo na samani vitabu mihtasari ya masomo na vifaa vya kufundisha na kujifunzia na kuajiri walimu na wafanyakazi wengine wenye sifa na uzoefu.
ii. Mwenye Shule ambaye Shule yake imetimiza vigezo vyote na shule kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Kanda hupewa taarifa ya kusajiliwa kwa Shuleyake kimaandishi. Aidha, atapatiwa cheti cha usajili chenye namba ya usajili wa shule.

iii. Usajili wa shule za serikali kuanzia Awali, msingi na Vituo vya Elimu ya Watu wazima unafanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya/Manispaa na hatimaye Wizara hupatiwa taarifa ju ya usajili wa shule na vituo hivyo.

Usajili wa Shule za Kimataifa

i. Wizara husajili Shule za hadhi ya Kimataifa, usajili huo unafanywa na Taasisi za Kimataifa zinazosajili shule za aina hii.
ii. Wizara huthibitisha na kutambua shule zinazosajiliwa na taasisi hizo kama za kimataifa. Taasisi hizo ni European Concil for International School ("E.C.I.S.) na "Association of Internation School in Africa" (AISA). Taasisi hizo zimeweka vigezo vya kusajili shule za kimataifa na shule itapewa usajili pale tu itakapotimiza vigezo vyote vilivyowekwa.

Hatua za kufuata ili Shule iwe ya Kimataifa

Mwenye Shule ye yote anayetaka Shule yake iwe na hadhi ya kimataifa anapaswa kufuata hatua zifuatazo:

i. Shule isajiliwe na wizara kama shule ya kawaida.
ii. Mwenye shule na aiombe wizara kimaandishi kutaka shule yake iwe ya kimataifa.
iii. Endapo wizara itaridhika na ombi hili itatoa kibali cha maandishi na mwenye shule ataendelea na hatua za kutuma maombi kwenye taasisi zinazosajili shule hizo.
iv. Shule itakaposajiliwa kama shule ya kimataifa, mwenye shule aijulishe wizara kimaandishi na kuambatisha nakala za usajili huo.

Usajili wa Shule au Taasisi za kidini

Taasisi za kidini zinazotaka kuanzisha na kuendesha shule/taasisi za kidini zinapaswa kufuata hatua zote tatu kama zilivyoelezwa isipokuwa wanapaswa kujaza fomu Na. RS. 9 katika hatua ya usajili.

Tanbihi

Uvunjaji wa sheria kwa namna yo yote ile ni kosa la jinai na adhabu yake ni kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 kifungu cha 59. Serikali ya Kijiji inahusika na mchakato wa usajili wa shule za serikali. 43

Mfano wa Uandishi wa Maombi Kujenga Shule ya Sekondari

(Anuani ya Mwombaji)

Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S. L. P. 9121
**DAR ES SALAAM**
K.K.
Afisa Elimu Mkoa
S. L. P. 901
**DODOMA**
K. K.
Afisa Elimu Wilaya
Elimu ya Secondari
S. L. P. 11
**KONDOA**

**YAH:**

1. Kibali cha kujenga shule ya Sekondari.
2. Kutwa/Bweni
3. Wavulana/Wasichana au mchanganyiko
4. Mchepuo wa sayansi
5. Mahali
6. Mradi wa nani
7. Mfadhili
8. Sababu ya kuanzisha shule (Huduma za kijamii afya)
9. Ukubwa wa eneo – ekari 12 ......
10. Watakaofaidika ya huduma: – wanakijiji, ... Watanzania.

(Mwombaji)
(Wasifu)

## REJEA


- Mwongozo wa kanisa Toleo la 18 (2010)
- GC and ECD, Seventh-Day Adventist Church Working Policy (FE) (2007)
- Mwongozo wa idara ya elimu kwa wachungaji, wazee wa makanisa na waratibu wa elimu kanisani UNION YA KUSINI MWA TANZANIA.
- Mwongozo wa Wizara ya Elimu TZ.
- Mwongozo wa Idara ya Elimu katika jimbo la NYANZA KUSINI na MWL ISAACKS MANYONYI (2016)
- Rejea za vitabu vya sifa za mwalimu zimenukuliwa toka katika vitabu vya Ushauri kuhusu Elimu vilivyo katika lugha ya kiingereza:
    - Elimu ya Kikristo (Christian Education: CE),
    - Ushauri kwa wazazi, walimu na wanafunzi (Counsels to Parents, Teachers and Students: CT)
    - Elimu (Education: Ed),
    - Misingi ya Elimu ya Kikristo (Fundamentals of Christian Education: FE

South Nyanza Conference
Idara ya Elimu
©2023